

HALIUZWI

APRIL - JUNE 2019

femba



**THE POWER
OF LOVE**

**MWONEKANO
WA
MAFANIKIO**

**THE
MAFIK**

**ART &
CELEBRATION**

**MISINGI
YA SANAA**

**TICHA
MC**

Jifunze Jipange Wajibika

NMB inakuletea elimu ya masuala ya kifedha inayoitwa - WAJIBU. Wajibu ni program maalum inayompa mzazi, mtoto na kijana fursa ya kujifunza masuala ya kifedha ikiwa ni pamoja na kujifunza mbinu za kuweka akiba kwa maisha yao ya baadae.

BWANA SAMA NA MKEWE BI BAHATI NI WAKAZI WA KIJIKI CHA WAJIBU BI BAHATI NI MAMA WA NYUMBANI NA MUMWE ANAJISHUGHULISHA NA KAZI ZA UJENZI



BWANA SAMA NA MKEWE WANA MTOTO MMOJA AITWAYE UHURU



RAFIKI YAKE MKUBWA NI JOHARI, WANASOMA DARASA MOJA.



BABA YAKE JOHARI NI FUNDI SEREMALA



WAZAZI WA JOHARI NA UHURU MARA NYINGI HUSIKIA KUHUSU BENKI NA VYAMA VYA KUWEKA NA KUKOPA



HIVYO KWA KIDOGO WANACHOPATA HUKITAHIDI KUWEKA AKIBA KWA AJILI YA ELIMU YA WATOTO WAO



UHURU NA JOHARI WANASOMA KWA BIDII ILI WAVEZE KUWA NA MAISHA BORA



SISI KWA PAMOJA TUMENUIA KUFIKIAMALENGO YETU



WAJIBU
SAVINGS

Jifunze, Jipange-WAJIBIKA!

Dear Reader

This issue is about 'Art and celebration' and the incomes we can generate through expressing ourselves in artistic ways.

At Femina Hip we recently celebrated our 20year anniversary and we hosted a big party for our 'femina family' members, our many contributors and partners through the years. We wanted to share the story of our journey and commemorate the work that we have done to build the Femina media platform. We also wanted to sparkle with joy in the Femina way, using Art and Entertainment. The party was a heartwarming and memorable event. Read the cover story, the 'Power of Love' about The Mafik, the band that entertained us throughout the night and lifted our spirits to the sky!

At the party, the Diamond Jubilee hall sparkled! It was decorated with colorful Art and designs, and you can see the photos on the Fema Club pages! Many awards were given out and a key attraction was the Femina fashion show which had team members wearing their own khanga outfits! It's true, dressing up is definitely about expressing our identities, so in the ChezaSalama article you can read all about 'dressing for success'. But what is a party without an MC, we had our beloved Amabilis. However, there are artistic and talented MC's out there so read the backcover story where Baraka Bihurugu talks about his MC work. He is a Fema club mentor making use of his talent!

Any celebration these days has to be documented with photography for memory sake. With social media and mobile phones the skill of taking photos is spreading. Meet Albert Mbepera who works as a professional photographer and talks about making a career of his passion.

So! There are many types of expressive Art, it surrounds us in society and frames our lives. In Tanzania the sector is regulated by BASATA. We explain how they work with artists in the Sema Tenda article, as all artists have to register with them.

The Art sector has lots to offer and the Art industries are growing, there are jobs and income opportunities to be found. Do you have artistic talent? Have a good read, find out more!

Pata mastori kuhusu sherehe za miaka 20 ya Femina

Na pia tunazungumzia tasnia ya sanaa na ubunifu



EXECUTIVE DIRECTOR

Dr. Minou Fuglesang

MEDIA DIRECTOR

Amabilis Batamula

MEDIA PRODUCTION MANAGER

Tunu Yongolo

SENIOR EDITOR

Pendo Mashulano

PHOTOGRAPHERS

Raphael Nyoni

K15 Photos

CONTRIBUTORS

Nashivai Mollel

Constancia Mгимwa

Gloria Mkoloma

Bahati Mdetele Nyembe

Sekela Mwaipaja

Haridi Issa

Geoffrey Machemba

Hija Shante

Zauja Mohamed

Asha Maneno

COVER PHOTOGRAPHY

Raphael Nyoni

LAYOUT DESIGN

Alison Bush

Julie Turgeon

Stephen Makoga

CARTOONS

Babatau, Inc.

DISTRIBUTION

EAM Logistics Ltd.

PRINTING

Jamana Printers

This issue of Fema is made possible by the generous support of the Governments of Sweden (Sida) and Denmark (DANIDA).

The contents are the responsibility of Femina Hip and do not necessarily reflect the views of the sponsors.



SWEDEN

EMBASSY OF DENMARK

DANIDA INTERNATIONAL DEVELOPMENT COOPERATION

COVERSTORY



THE MAFIK:

THE POWER OF LOVE

NA TUNU YONGOLO





Sote tuligubikwa na furaha baada ya Mkutano wa Vijana wa Femina mwaka huu ambapo mimi na Fema clubbers wengine tulipata fursa ya kuhudhuria sherehe za maadhimisho ya miaka 20 ya Femina! Wow, wengi wetu sisi wanafunzi tuliotoka shuleni sehemu mbalimbali za nchi hatukuwa tumewahi kuhudhuria party kubwa kama ile. Ilifanyika katika ukumbi wa Diamond Jubilee, mapambo yalikuwa kiboko, maonyesho ya mitindo ya mavazi yaliyofanywa na wafanyakazi wa Femina yalinoga balaa, catwalk ndo usiseme, tuzo zilikuwa za kumwaga na kwakweli zilileta furaha, kama hiyo haitoshi, kulikuwa na live performance matata kabisa, walipanda stejini wasanii maarufu nchini Tanzania, Bendi ya The Mafik – walitisha! Watu walikaa katika meza kubwa za mviringo na kila kona ilikuwa inafikika kwa urahisi. Tulipiga stori na watu kibao, wanafamilia wenzetu wa Femina na hata wazungu na viongozi wakubwa serikalini, mawaziri ambao walikuja kuungana na Femina katika maadhimisho hayo.

We were all dizzy with excitement, after the Annual Youth Conference this year, I and other Fema clubbers got to participate in the Femina 20 year party! Wow, most of us clubbers from schools across the country had never been to a big party like that. It was held in the Diamond Jubilee Hall, the decorations were spectacular, the Femina team's fashion show on the catwalk was a blast, the Awards, many and heartwarming and the live performance on stage from one of Tanzania's most well-known bands - The Mafik - was amazing. People were seated around big round tables and everyone was so accessible. We talked to many of our fellow 'Femina family' members and we even met some 'muzungu' foreigners and 'big people', government ministers who had come to celebrate the anniversary.



Bendi ya the Mafik ilipiga nyimbo tatu pendwa usiku ule, wimbo mmoja walishirikiana na msanii Barnaba!! Hawana uchoyo na mic, walitoa nafasi kwa watu kupanda jukwaani na kuimba pamoja nao, tena hatutomsahau Mu Rapper, Fema Clubber kutoka Tanga, alikwea jukwaa akakamata mic na kutoa burudani moja kali. Alituburudisha kwa rap yake iliyohusu Fema Clubs. Ilikuwa inafurahisha namna The Mafik walivyotoa fursa kwa vijana kuonyesha vipaji vyao jukwaani. The Mafik walisambaza upendo usiku ule. Hebu tuwafahamu zaidi The Mafik. Ni akina nani hawa na walianzaje harakati zao za muziki?

The Mafik, jina ambalo limetokana na maneno 'Maendeleo, Fikra Pevu na Kazi', ni kikundi cha vijana watatu kilichoundwa mwaka 2016. Vijana hao ni Rhino (28), Mbalamwezi (26) na Hamadai (27). Wote hawa wamekuwa waimbaji katika maisha yao yote lakini wakagundua kwamba wana sauti na staili ya Bongo Flava ambayo inaendana, hivyo wakaamua kuunda bendi pamoja. Kundi hili limevuma zaidi kwa nyimbo zao Passenger na Niwaze (ambayo waliimba na Ruby), Sio mbaya (walimshirikisha Ben Pol), Karola, Sheba na Dodo; nyimbo ambazo zinahusu mapenzi na mahusiano. Wanatueleza kuhusu nguvu ya 'teamwork' na jinsi wanavyoshirikiana katika majukumu yao yote na kazi zinazohusu kutengeneza muziki!

The Mafik band performed three popular songs during the party night, and one of them was with the famous Barnaba!! They invited the audience to come up and sing with them and we can't forget the Fema clubber, Mu Rapper from Tanga, he was so impressive and entertained us by rapping about Fema clubs. It was so exciting that they gave a chance to talented youth to perform. The Mafik helped to spread the 'power of love' that evening. So, who are they and how did they start their journey into music?

The Mafik, which stands for 'Maendeleo, Fikra Pevu na Kazi', is a group of three formed in 2016, namely Rhino (28), Mbalamwezi (26) and Hamadai (27). All of them have been singing all their lives but found that they had a sound and Bongo Flava style that matched, so decided to form a band together. The group is well known for the songs Passenger and Niwaze (which they sang with Ruby), Sio mbaya (featuring Ben Pol), Karola, Sheba and Dodo; songs about love and relationships. They talk to us about the power of teamwork and how they share all the responsibilities and tasks involved in making music!

Rhino and Sekela from girl power team performing together



Hamadai akifanya vitu vyake.



Mbalamwezi akitamba jukwaani



Drums nazo zilibamba sana tu.

Hii inamaanisha kwamba Rhino, Hamadai na Mbalamwezi wote kwa kushirikiana wanaandika mashairi, wanapiga baadhi ya vyombo vya muziki na wote wanaimba. Bendi hii ni gumzo mjini. Kwa sasa muziki wao unapigwa redioni na wamekuwa wakifanya show katika matamasha makubwa ya muziki kama Tigo Fiesta Singida, Dodoma na Dar es Salaam, Tamasha la Kimataifa la ZIFF linalofanyika Zanzibar pamoja na tamasha la Komaa jijini Dar es Salaam. Tunashangaa wamewezaje kufika mbali namna hii katika nyanja ya muziki?

Rhino anaeleza kwamba tasnia ya muziki ina faida na pia ina changamoto zake. Kwa mfano, kuna fursa nyingi za kufanya show, lakini kipato wanachokipata wanamuziki walio wengi hakitoshi kumtajirisha mtu. Unapaswa kuwekeza 'jasho la damu na machozi' kama wasemavyo, na ni lazima ukipende kile unachokifanya. Gharama za uzalishaji ziko juu, unapoanza unahitaji vifaa lakini kipato unachokipata kwa 'kuuza' muziki hakilingani na kiasi unachowekeza. Hata hivyo, uzuri wa kuwa mwanamuziki ni ile hali ya kufurahiwa na hadhira na fursa ya kufika sehemu mbalimbali, kukutana na wasanii wengine na kujenga mtandao wa watu.

This means Rhino, Hamadai and Mbalamwezi all write the lyrics, play some instruments and they are all vocalists. They are hot right now, their music is heard on radio and they have been performing at music festivals such as Tigo Fiesta in Singida, Dodoma and Dar es Salaam regions, Zanzibar International Festival (ZIFF) as well as the Komaa Concert in Dar es Salaam, etc. We wonder, how did they make it this far in the music business?

Rhino explains that the music industry has both benefits and challenges. For example, there are many opportunities to perform, but the money most musicians earn is not enough to make you rich. You have to invest a lot of 'blood sweat and tears' as they say, and you have to love what you do. The cost of production is high, you need equipment and instruments to start but still the income that comes from 'selling' the music doesn't always match the investment. However, the most rewarding part of being a musician is feeling the love from the audience and getting the exposure, meeting other artists and networking.



Mbalamwezi anaongeza kwamba kila mwenye kipaji na ambaye anataka kuendeleza kipaji chake anahitaji meneja. Huyu ni mtu mwenye utaalim unaohitajika na ambaye anaweza kukusaidia kukupatia mwongozo ili ujue nini cha kufanya na nini cha kuepuka katika kuendeleza kipaji chako na namna unavyoweza kushirikiana na wanamuziki wengine kuunda bendi. The Mafik kwa sasa wanasimamiwa na meneja wao Michael Mlingwa, maarufu kama Mx Carter. Pia ni meneja wa wasanii wengine maarufu kama Shetta, Damian Soul, Shilole na Barnaba.

The Mafik wanafahamika kwa kutoa nafasi kwa hadhira kupanda jukwaani na kuimba pamoja nao. Wanasema kwamba, kama mwanamuziki, unapaswa kuwa na uwezo wa kuwasiliana na hadhira, kuwaonyesha upendo na kuonyesha shukrani kwa kuwa pamoja nawe. "Hadhira ndiyo inayotufanya tupendwe na kupata umaarufu. Ni kwa kufurahi kwao ndipo tunajenga jina. Ndoto ya The Mafik ni kuanzisha kituo cha kuwafundisha vijana muziki. "Tungependa 'kushea' mapenzi yetu ya muziki na kufundisha muziki kwa vijana wa kizazi kijacho. Kuna mengi ambayo mnapaswa kuyafahamu kuhusu tasnia ya muziki, taratibu zake na namna ya kujitengenezea kipato kutokana na muziki."

"Maisha ni vile unavyoyajenga" Rhino anahitimisha. "Maisha yako ni yako, sio ya mtu mwingine. Jipange vizuri ili uishi maisha unayoyataka. Unapaswa kuamini kwamba hakuna kisichowezekana. Hupaswi kukaa ukisubiri msaada. Jikomboe. Ni jukumu lako kuithibitisha dunia kwamba una kipaji."

"Ndiyo! Unapaswa kuchapa kazi kana kwamba maisha yako yanategemea kipaji hicho, kwasababu ni kweli kwamba maisha yako yanategemea kipaji chako." Mbalamwezi anaendelea kusema. "tafuta ujuzi unaotakiwa ili upate mafanikio. Umaarufu hauji ghafila. Na siku zote juhudi zinalipa. Siku zote."



**Mussa H Ally aka Mu Rapa
Mwana Fema kutoka Tanga
akitoa burudani**

Mbalamwezi adds that everyone who has talent and wants to take it out there needs a manager. This is someone with the right expertise and who can assist with mentorship so that you learn what to do and what no to do to develop your talent and how you can work with other musicians to form a band. The Mafik are currently under the management of Michael Mlingwa, known as Mx Carter. He is also the current manager of other famous artists such as Shetta, Damian Soul, Shilole and Barnaba.

The Mafik is known for inviting members of their audience to joined them on stage to sing. They explain that as a musician, you need to be able to communicate with the audience to show them love and appreciation as they in return engage with you. "It is the audience who make us loved and famous. It is through their happiness that we become who we are. The Mafik dream about opening a centre that can coach and educate other youth about music. "We would like to share our love of music and coach the next generation of youth. There is a lot you need to know about the music industry, the rules and how to make an income from sharing your music."

"Life is how you make it" Rhino concludes. "Your life is yours and no one else's. Put on your shoes and gear yourself to live the life you want. You have to believe that nothing is impossible. You cannot wait for help. You have to be your own savior. It is your duty to prove to the world that YOU have the talent."

"Yes! You have to work as though your life depends on it, because in many instances, it actually does." Mbalamwezi carries on. "Acquire the knowledge that is needed to succeed and remember, fame doesn't come overnight. But hard work always pays. Always."



**Barnaba naye alijumuika
na The Mafik**

Miaka ishirini ya kibabe!



Shughuli ni watu na watu wenyewe ndio sisi, Miaka 20 si mchezo!

Ukumbi wa Diamond Jubilee uliwaka kwa vicheko, sura zenye tabasamu, shangwe na vigelegele wakati wafanyakazi wa Femina wakikatiza jukwaani na mitindo mbalimbali ya mavazi waliyobuni ili kusherehekea miaka 20 ya Femina. Si unacheki mwenyewe hizo sura zilivyo na bashasha.



FEMINA FAMILY FESTIVAL



Haiwezi ikawa shughuli bila 'makulaji' na 'makunywaji'. Wageni rasmi walikata keki ambayo iligawiwa katika kila meza na kila mtu alipata kipande chake cha utamu wa miaka 20 ya Femina. Madikodiko mengine acha kabisa, ilikuwa ni full kujilamba.





Kwa mara nyingine Waziri wa Afya, Umy Mwalimu alirudia kauli aliyotoa Tanga, kwamba angependa kuona kila shule nchini ina club ya Fema. Big up sana kwa wana Fema club mnafanya makubwa ambayo yanamvutia hata mheshimiwa na kutamani kuona shughuli za club zimetapakaa Tanzania nzima.



Maonesho ya kazi za Fema clubs.



Richard Mabala mwandishi wa kitabu cha Mabala the Farmer pia alikuwepo.

Picha za kumbukumbu zilipigwa kwa kila mtindo.



Waliong'aa zaidi 2018!

Mambo vipi? Kama inavyofahamika, kila mwaka tunatoa tuzo kwa wote waliong'aa zaidi katika mwaka huo. Kwa 2018 tuzo zilitolewa katika ule usiku wa kusherehekea miaka 20 ya Femina. Kila mmoja shauku ilikuwa juu sana. Na hapo ndipo mshereheshaji wetu alipoanza kuwaita jukwaani ili wakabidhiwe tuzo zao.



Best Fema Club Mentor SOPHIA A. JUMA

Huyu ni jembe wa Murad Saddiq Fema Club kutokea mji kasoro bahari, Morogoro. Ilikuwa ni 'surprise' kubwa mno kwa upande wake maana hakuwa anajua kabisa kuwa atanyakua 'taji' hili. Makofi ya nguvu kwa madam Sophia! Alisogea kutoka alipoketi kwenda kupokea tuzo yake kwa furaha isiyoelezeka, kila mmoja alimshangilia. Alipokamata tu tuzo yake na kurudi katika eneo lake nikamuwahi na kuanza kuzungumza naye. "Nimegundua kuwa mafanikio huja kidogokidogo na inabidi tusikate tamaa. Tangu 2013 nafanya kazi za Fema bila kupata tuzo yoyote, wala club yangu haikuwahi kutokea kwenye jarida lakini sikukata tamaa," aliniambia.



Best Fema Club – MISUNGWI

Ukumbi mzima ulitawaliwa na nderemo! Wengine wanaulizana, tena? Hahaha! Hawa jamaa siyo mchezo, hawana utani kabisa katika shughuli zao. Mwaka jana waliibuka club bora, wakaona haiwezekani kuachia kijiti hiki, wakapambana tena, wakawa wabunifu zaidi, wakawa wajasiriamali na kuibeba vyema bendera ya Ruka Juu katika shughuli zinazowajengea stadi na mbinu za kutengeneza kipato. Walianza kutengeneza bidhaa kama vile jam, karanga, ubuyu, juice ya maganda ya nanasi na mbolea. Usisahau vile viwanda vidogo vya pads, chaki na ile ofisi yao ya chupa za plastiki, vyote bado vipo.

Hakukuwa na namna zaidi ya kuwapa wao tena tuzo. Clubs zilizofanya vizuri ni nyingi lakini walibaki kuwa 'the best'. Kama kawaida, nikamdaka mlezi, Mwalimu Kahwa Anacleth Mpunami ili anipe mawili matatu. Yeye alinikumbusha kaulimbiu yao "Don't tell people about your dream but show them". Walikuwa wana ndoto ya kuwa club bora kwa muda, 2017 walituoonesha mafanikio, 2018 wakayasisitiza. Pongezi za nguvu kwenu Misungwi. "Misungwi ya Viwanda Inawezekana".

Best Network of Fema Clubs – TANGA

Sifa kuu ya hawa jamaa ni umoja. Kuthibitisha hilo, waliandaa matamasha kila wilaya na mwishowe wakafunga kwa tamasha kubwa la ngazi ya mkoa ambalo lilihudhuriwa na watu zaidi ya elfu moja na mgeni rasmi alikuwa ni Waziri Ummu Mwalimu. Hawa jamaa pia ni wabunifu sana. Wametengeneza kalenda zao na zinavutia sana. Pia wamehakikisha uanzishwaji wa club mpya na kufufua zile zilizokuwa zimelala, ili kuthibitisha kuwa Fema clubbers ni vijana wa kuigwa, wameanzisha kampeni ya kutokomeza 'zero'.



Second Best Network of Fema Clubs – KAGERA

Wako juu sana hawa. Walionesha moto wao kwa kuandaa matamasha mbalimbali ambayo yote yalifana sana. Walifanya usafi katika maeneo ya umma kuhakikisha mazingira yanakuwa rafiki. Hawa pia walianzisha harakati za kutokomeza sifuri, na kubwa zaidi, waliandaa maandamano ya kupinga ukatili wa kijinsia, wakishirikiana na jeshi la polisi. Lengo lilikuwa ni kufikisha ujumbe kuwa ukatili wa kijinsia haukubaliki kwenye jamii yetu.



Best Fema Club Network Mentor ELIUD KABENGO

Huyu ni mentor wa Simiyu Network of Fema Clubs. Yeye alihakikisha shule ambazo hazina club za Fema mkoani Simiyu zinaanzisha club na sasa zinapokea majarida. Lakini pia alihamasisha club zilizolala kuamka, alihakikisha club hizo zinajiunga katika network za wilaya na mkoa. Hakuishia hapo, aliaandaa mafunzo ya kujifunza kwa kushiriki yaani Active Learning mkoani Simiyu na alisaidia kuunganisha Fema clubs za wilaya ya Maswa na mamlaka za wilaya hiyo na hatimaye alifanikiwa kumpata Katibu Tawala wa Wilaya ya Maswa kuwa mlezi wa network ya wilaya hiyo.



Femina inatoa pongezi nyingi kwa waliotwaa tuzo mwaka huu. Tunawapongeza pia walezi wote wa networks na walezi wa Fema Clubs. Tunafahamu kwamba wanaofanya vizuri ni wengi sana tu, lakini tunalazimika kuwapa tuzo wachache kwa niaba ya wengi. Jambo la muhimu ni kwamba kuwe na tuzo, kusiwe na tuzo, kazi ya kuzilea Fema Clubs tunaifanya kwa faida ya vijana wetu, jamii zetu na vizazi vijavyo. Hivyo kimsingi, sisi sote ni washindi.

20 ya Kibabe, Tuzo za Kibabe!

Najua umesoma na kusikia story nyingi kuhusu usiku wa miaka 20 ya Femina au kama tunavyopenda kuuita Birthday ya familia yetu. Usiku huu ulifunikwa na furaha na 'surprise' kibao. Unakumbuka shindano la Miaka 20, Washindi 20, Zawadi 20? Hili lilikuwa ni shindano la uandishi wa insha kuhusu miaka 20 ya Femina. Usiku huu ndipo washindi walikabidhiwa zawadi zao.



Kwa kweli, insha zilipokelewa nyingi sana, majaji walifanya uchambuzi wa kina na kati ya mamia ya watu waliotuma insha zao wakapatikana washindi ishirini. Sisi tunaamini kila mmoja alikuwa ni mshindi kwa sababu kila mmoja aliandika kutokana na uzoefu wake, lakini isingewezekana kuwapa zawadi wote.

Ngoja nikupe story sasa. Ndani ya ukumbi moto uliwaka na shangwe hazikuwa za kitoto ulipofika wakati wa kukabidhi zawadi kwa washindi hao. Washindi walikuwa kwenye makundi matatu, walimu walikabidhiwa Tablets aina ya Samsung, clubs zilikabidhiwa laptops na wanafunzi walikabidhiwa baiskeli zao. Zawadi zote zilikuwa mpyaaa! Yaani brand new!

Furaha ya washindi na nderemo hazielezeki, palikuwa hapatoshi ndani ya Diamond Jubilee. Naamini sasa hivi wanajivinjari na zawadi zao.

Msimko ulikuwa mkubwa kwa sababu ilikuwa ni bongwe la surprise kwa washindi.

Ili kuthibitisha kuwa walioshinda walistahili ushindi huo, tukaona siyo mbaya kama tutasoma insha mojawapo. Basi ilisomwa pale mbele ya umati na watu walikubali kuwa kweli Femina imegusa maisha ya watu. Bila shaka ulisoma majina ya washindi na insha zao katika toleo namba 50, toleo maalum la miaka 20 ya Femina Hip. Tuendelee kuwa moto!



Youth Conference 2019 kuli happen!

Ni aje Fema clubbers? Natumai mko poa na bukheri wa afya! Hapa nimejaa hamasa ile mbaya, nataka kukumegea japo kiduchu yaliyojiri kwenye Femina Hip Youth Conference 2019. Si unajua Youth Conference huwa inafanyika kila mwanzo wa mwaka? Mwishoni mwishoni hivi mwa mwezi Januari. Basi ya mwaka huu aiya-ya-ya-ya! ilikuwa ni fire, full kudamshi kisomi.



Nadiriki kusema Youth Conference ya mwaka huu ilikuwa ni ya kipekee zaidi kwa sababu iliungana na sherehe za kutimiza miaka 20 ya Femina Hip. Tulikutana Fema Clubs 64 zilizowakilishwa na wanaFema zaidi ya 150, kwa siku tatu, ndani ya Seascope Hotel, Dar es Salaam. Tukabadilishana uzoefu ili kuimarisha na kuboresha mazuri yanayoendelea kufanyika katika club zetu.

Nondo za kutosha!

Jumatatu ya Januari 21 ilikuwa ni shughuli ya kuwapokea wanaFema kutoka mikoa yote ya Tanzania. Baada ya wageni wote kuwasili tulikaribishana na kupeana ABC's za kipindi chote tutakachokuwa pamoja. WanaFema ni wanaFema tu, japokuwa walitoka mikoa mbalimbali lakini unaweza ukadhani walitoka shule moja kwa jinsi walivyojenga urafiki fasta.



Zawadi kutoka Ashira Fema Club



Uchangamfu ulikuwa ni wa hali ya juu na hata muda wa vipindi ulipoanza haikuwawia vigumu wawezeshaji kuendesha mada mbalimbali. Kwa siku tatu mfululizo ilikuwa ni kupigana msasa katika stadi mbalimbali za maisha. Maeneo yaliyogusiwa ni kama vile utoaji wa ushauri nasaha, jinsi ya kuandaa maigizo na uigizaji, masuala ya ukatili wa kijinsia, elimu ya uwezeshaji wa kiuchumi, elimu ya uraia, matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii pamoja na utoaji ripoti kwa shughuli za club. Wawezeshaji wakuu katika maeneo yote haya hawakuwa wengine bali ni wafanyakazi wa Femina. Wanaclub walipata nafasi ya kufanya kazi katika makundi na kisha kuwasilisha maoni yao mbele ya wenzao. Power Teams nao walikuja ku-share stori zao ili kuwahamasisha wana Fema kufanya vizuri zaidi katika masomo yao. Haikuwa hivyo tu, bali mipango mikakati ya kuboresha utendaji wa club zetu iliwekwa ili kuhakikisha kwa miaka ijayo tunafika mbali zaidi.



Bata kama lote

Madarasa hayakuwa kama shule kwamba ni pindi baada ya pindi. Kulikuwa na break time, ambapo tulipata chai na bites za nguvu. Wasaa huu pia wanafunzi walipata nafasi ya kuandika ujumbe na kubandika katika ukuta maalum, kupiga picha za kumbukumbu na hata kujenga marafiki wapya. Ratiba ya madarasa ilikuwa inakwisha saa kumi na moja jioni, na baada ya hapo ni kujimwaga katika michezo ya

ufukweni ili kujenga afya na kuchangamsha akili. Michezo kama kukimbia na magunia, mbio za vijiti, na kuvuta kamba ilibamba vilivyo. Halafu kukatokea mchuano kati ya walimu na wanafunzi katika kuvuta kamba, hata sikumbuki nani alishinda aisee! Walimu waliondoka wanashangilia hali kadhalika na wanafunzi. Ikawa burudani ndani ya raha. Unajua nini, nikiandika zaidi kurasa hazitatoshwa, wacha niishie hapa. Fema Clubs hapana chezea.



Tuzo Mkoa kwa Mkoa



Kama kawa kama dawa. Tuzo za Club Bora kwa kila mkoa nazo zimeendelea kuunguruma, sambamba na tuzo nyingine.

Clubs zilizochukua tuzo ni zile ambazo zimeonesha ufanisi mkubwa ndani ya mwaka mzima. Walikuwa wakifanya shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii, ukiacha shughuli ya msingi kabisa ambayo ni kusoma, kujadili na kutekeleza yaliyomo ndani ya jarida la Fema. Hebu fuatilia ujue nani kapanda, nani kashuka, nani kabaki palepale. Karibu!

| | |
|---------------|-------------------------|
| Arusha | Sakila Fema Club |
| Tanga | Old Tanga Fema Club |
| Kilimanjaro | Mji mpya Fema Club |
| Mwanza | Sengerema Fema Club |
| Mara | Kemakorere Fema Club |
| Simiyu | Ibulyu Fema Club |
| Shinyanga | Tinde Fema Club |
| Kigoma | Kigoma Grand Fema Club |
| Kagera | Ihungo Fema Club |
| Geita | Nyakamwaga Fema Club |
| Katavi | Magamba Fema Club |
| Rukwa | Mkangale Fema Club |
| Njombe | Maria Nyerere Fema Club |
| Songwe | J.K. Nyerere Fema Club |
| Ruvuma | Londoni Fema Club |
| Iringa | Selebu Fema Club |
| Mbeya | Ngonga Fema Club |
| Morogoro | Murad Saddiq Fema Club |
| Lindi | Mnonela Fema Club |
| Mtwara | Maundo Fema Club |
| Pwani | Zinga Fema Club |
| Manyara | Gitting Fema Club |
| Dodoma | Farkwa Fema Club |
| Singida | Shelui Fema Club |
| Tabora | Nanga Fema Club |
| Dar es Salaam | Saku Fema Club |



Ingawa hawa ndio walioibuka na tuzo, lazima tukubaliane na ukweli kuwa clubs zinazofanya makubwa ni nyingi sana. Kwa ufupi tuseme sisi sote ni washindi. Tuzo ni motisha kwa waliopokea na wengine wote. Waliopata kwa mwaka 2018 ndiyo hao hapo juu, kipenga kimepulizwa tena kuashiria kinyang'anyiro kimenza upya. Walioshinda watataka kutetea ubingwa na ambao hawakupata tuzo wanahitaji kupata. Twende kazi!



Kumi wanyakua tuzo maalum

Fema Club mentors wanapiga kazi mpaka tunadata! Walezi hawa baadhi yao waliwahi kupata tuzo mbalimbali lakini kupata kwao tuzo hakukuwafanya walale, badala yake imekuwa ni chachu kwao kuendelea kuchapa kazi.

Wapo baadhi yao ambao hawakuwahi kupata tuzo lakini wamekuwa wakifanya vitu extraordinary kwa zaidi ya miaka miwili bila kusimama! Basi tukasema, hebu nasi tuanzishe tuzo extraordinary! Hii ni tuzo maalum kwa watu maalum kwa kutambua mchango wao maalum katika kuliungurumisha gurudumu la Femina na Fema Clubs.

Waliotunukiwa tuzo hii maalum 2018 ni hawa wafuatao.



Washindi katika picha na baadhi ya wafanyakazi wa Femina





Adam Matimbwa

Adam ni mlezi wa Mnero Fema Club iliyoko Mkoani Lindi. Yeye anapambana kukuza vipaji vya wana Fema Club katika mambo kibao ikiwemo kuimba, kucheza na kuigiza. Hajaishia hapo, na katika sekta ya kilimo pia yupo gado, anawasapoti wanafunzi wake.

Adam ni moto!



Mejah Matu Kamura

Huyu ni Mwenyekiti wa Serengeti Network of Fema Clubs. Alipambana vilivyo hadi kuhakikisha walezi wa Fema Clubs za Serengeti wanapata mfidhili wa kuwalipia gharama za kuhudhuria mkutano wa kitaifa wa Fema Club Mentors uliofanyika Mwanza, 2018. Kamura amehakikisha ofisi za elimu wilayani Serengeti zinatambua mchango wa kazi za Femina katika jamii.

Big up sana!



Renatus Sangi

Ni mlezi wa Iringo Fema Club na pia ni mwenyekiti wa Mara Fema Club Network. Sangi alipita kila kona akihamasisha kuundwa kwa network za wilaya na hatimaye mkoa mzima wa Mara umeungana.

Sangi, uko juu vibaya mno!



Mayombo C Lutego

Huyu ni mwanzilishi wa Tanga Fema Club Network. Amekuwa akitembelea shule kwenye halmashauri na kuanzisha Fema Clubs. Pia ana ushirikiano mkubwa sana na mitandao mingine ya Fema Clubs na amekuwa akitembelea clubs kona kibao za nchi bila kujali umbali. Ni mhamasishaji wa shughuli za uzalishaji mali.

Mayombo, uko vizuri sana. Hongera!



Sifa Samson Sizya

Sifa ni mlezi wa Chang'ombe Sec Fema Club. Ni rafiki mkubwa wa wanafunzi na mtetezi wa usawa wa kijinsia. Miongoni mwa aliyoyafanya ni kushawishi uongozi wa shule kuweka sketi za akiba pale shuleni ili mwanafunzi atakayechafua sketi awapo hedhi aweze kujisitiri na kuendelea na masomo.

Sifa, chukua tano!



Elias John Matung'hingi

Ni mlezi wa Mambwe Fema Club na Mwenyekiti wa Rukwa Fema Club Network. Amewaongoza vijana kuanzisha mradi wa nyuki hivyo wanarina asali na kuuza. Ni msimamizi mzuri wa michezo na sanaa ambapo kwa kushirikiana na wanafunzi wake, wanaandaa mashindano ya soka na mshindi anatwaa mbuti. Pia amewezesha kuwepo kwa duka la Fema shuleni hapo.

Tisha sana mtu wangu!



Rabi Lubinza

Rabi ni mlezi wa Mwenge Fema Club iliyoko Singida. Shule yake ina wanafunzi wa kiume tu lakini amewajenga kutokusema kazi fulani ni ya kike au ya kiume. Wanafunzi wake walianza na bustani ya mbogamboga ambapo wamekuwa wakiuza mboga hizo shuleni na kuwapatia mtaji katika shughuli za mapambo. Pia amewafundisha kutengeneza kazi za sanaa kama vile mikoba, mazulia, mikufu n.k. Wanajifunza ujuzi thabiti.

Rabi, unatisha!



Emmanuel Msemakweli

Ni mlezi wa Guta Fema Club, ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Bunda (Mji). Japokuwa shule yake haikuwa katika program ya shule zilizochaguliwa kupata mradi wa Nguvu ya Binti, Msemakweli aliona faida za mradi huu, akaomba kuutekeleza shuleni kwake. Pia amekuwa akihamasisha kuanzishwa kwa Fema Clubs katika shule nyingine na kupiza ushirikiano pamoja na kuamsha clubs zilizolala.

Tisha sana bro!



Christopher Mavunde

Mavunde ni mlezi wa City Fema Club ya Dodoma na pia ni Mwenyekiti wa Mtandao wa Walezi wa Fema Clubs Tanzania. Kwa ufupi ni boss kubwa! Mavunde anaibua na kuongoza mijadala ikiwemo mijadala kutoka kwenye majarida kupitia Mentors Facebook Group, ni mwepesi wa kutekeleza jambo. Anajitoa sana! Anafika sehemu kibao za nchi bila kujali umbali, akihamasisha Fema Clubs kuwa active.

Mavunde, wewe ni jembe!



Kahwa Anaclet Mpunami


Kahwa ni mwanzilishi wa Club ya Fema Kagunguli Sec iliyo chini ya Kanisa Katoliki. Hata alipohamishiwa Misungwi Sec alipambana akaanzisha tena Misungwi Fema Club na kuhamasisha wanafunzi wake kujenga nyumba kwa kutumia taka za chupa za plastiki. Amefanya mambo kibao, ikiwemo kuwaongoza vijana kuanzisha kiwanda cha juice, jam, dawa ya mbu na mbolea ya maji.

Kahwa uko juu kinoma!

Tuongane kutoa pongezi kwa 'majembe' yetu haya kumi, na kwakuwa tuzo hii sasa imeanza rasmi, itakuwepo kila mwaka, basi tuchape kazi, tukutane tena 2019.

ART AND CELEBRATION!

Art is communication and it is created with imagination and skill. It expresses important ideas or feelings. Art appeals to us, it catches our attention, it pulls us in and opens us up to messages. Art is vital to all cultures and societies. Through Art we articulate our innermost concerns, dreams and longings even belongings, e.g. the colorful khanga with wording which is used by women in Tanzania, the jewelry of the Masaai, the white dress of the Christian bride, the baggy pants of the hip hoppers.



Left

DID YOU KNOW?

That our brain is divided into two parts: The LEFT side and the RIGHT side? The right brain controls the left side of the body and is the most artistic and creative side while the left brain controls the right side of the body and is more academic and logical. Isn't that interesting?





Art works are created by artists, who have artistic talent. It is said that those who are artistic have developed the right side of their brain! Art skills can also be learnt, there are training courses and schools to help you develop artistic talent. Art is industry, you can find markets for your Art and you can earn money from your Art. Art encompasses a diverse range of creations and expressions, including music and song; paintings, cartoons, sculpture, photography; drama, theater, comedy; literature, poetry and film to mention some.

There are different purposes for Art, one important is the Ceremonial use, celebrations are full of ceremonial. That is what we focus on in this issue of Fema magazine. This kind of Art is made to celebrate or commemorate something important in our culture, or worship, or in our personal lives.

During our lifecycle, depending on where we live, we have many rituals and celebrations to mark important days so that we can commemorate important events be they weddings, birthdays or deaths of our loved ones. We also celebrate religious occasions like the birth of Mohammed and Christ, or political markers like Independence Day, Saba Saba Day and Mwalimu Nyrere's birthday. These events help us create a sense of community and shared values - a sense of belonging.

At Femina we celebrated our 20year birthday this past January. We adapted the typical 'birthday' ingredients to fit us and the occasion. We invited all our family and friends, collaborators and donors and celebrated our accomplishments and growth over these past two decades. We framed it with Art – decorations using Fema logos, music, dance, awards of appreciation, khanga fashions and then of course the classic birthday symbol, the cake! The party was beautiful and created a memory that we will cherish for many years to come, it filled us all with love and gratitude!



MWONEKANO WA MAFANIKIO

NA FEMA TEAM PICHA: RAPHAEL NYONI

Tunavaa, tunatengeneza nywele zetu, wakati mwingine tunajipodoa. Mwonekano tunaouchagua unawawezesha wanaotutazama kufahamu sisi ni nani na tunataka kuwa nani. Mavazi ni jambo binafsi, ni sanaa kwani tunatumia miili yetu kama ubao wa kuchorea kuwasilisha ujumbe kwa wengine.

Nani alikufundisha namna ya kuvaa na kuchagua mtindo uliouchagua? Je, ni mtindo ambao unaufurahia? Sekela, mmoja wa wasichana katika timu yetu ya Nguvu ya Binti, anatusimulia stori yake.



Nilipokuwa na miaka kama kumi hivi, nakumbuka nilikuwa nikiamka asubuhi, namtazama mama anapojiandaa, tayari kuianza siku – anachagua nguo, anabana nywele zake na wakati mwingine 'anajipodoa'. 'Style' yake ilikuwa ikibadilika kutegemea matukio – anapokwenda kwenye ibada, anapokwenda harusini au sokoni kununua bidhaa kwa ajili ya duka lake. Nilikuwa nashangazwa na namna ambavyo anaweza kubadili mwonekano wake. Alipokuwa akivaa gauni tamu na kupaka lipstick nyekundu alionekana mwenye kujiamini zaidi na mchangamfu. Wakati mwingine alivaa nguo za heshima zaidi na alionekana mtaratibu, na wakati mwingine alivaa nguo nyeusi na hapo nilijua wazi kwamba mama hana furaha.

Nampenda mama yangu, aliniambukiza tabia yake hii na nafahamu kwamba mavazi ni jambo muhimu sana katika mwonekano wa mtu. Nilijifunza mapema sana kwamba jinsi unavyojiweka inaweza kuleta tofauti. Watu walimchukulia mama yangu kwa namna tofauti kulingana na jinsi alivyokuwa amevaa na ilimfanya ajisikie tofauti pia. Tangu wakati huo ingawa nilikuwa mdogo nilishapenda kuvaa vizuri, nilikuwa na gauni langu matata la njano ambalo nililipenda sana na lilinifanya niwe mwenye furaha kila nilipolivaa. Nilipokuwa shuleni nilivaa sare ya shule na nywele zangu ilibidi ziwe fupi muda wote. Hiyo haikunipa tabu, lakini nilisubiri kwa hamu siku nitakayohitimu masomo, nitakapokuwa huru kuvaa nguo nizipendazo na kutengeneza nywele zangu ninavyotamani! Nilitamani kuwa vile ninavyotaka na kujua nitaonekanaje nitakapojiweka vile ninavyotamani.



BEFORE



Haya ndiyo mambo ambayo Sekela alijifunza kuhusu mavazi:


Alifahamu UTAMBULISHO wake! Utambulisho ni nini? Ni kujua wewe ni nani. Ni mvulana au msichana? Je, wewe ni mwanafunzi? Ni kijana au ni mzee? Je, unatokea katika jamii ya aina gani? Utambulisho wako una mchango katika mwonekano wako – uvae nini, uonekaneje mbele za watu? Mavazi yanaweza kumsaidia mtu kufahamu wewe ni nani, kwanini umechagua mtindo fulani wa mavazi na ni namna ya kuwaelewa watu wengine vizuri. Maoni ya watu kuhusu mavazi tunayovaa pia ni muhimu. Unaweza ukavaa nguo ambayo itafanya kila mtu avutiwe kukutazama au ukavaa nguo ambayo itafanya watu hata wasigundue kama upo. Kama wewe ni binti kama Sekela, pengine utapenda sketi na magauni. Lakini, hebu tusijikite kwenye mazoea, wasichana wanaweza kupenda kuvaa suruali au nguo

nyingine ambazo si za kike wala za kiume. Unaweza kusuka nywele zako au kujiremba kwa 'nywele' za bandia, na mitindo mingine kibao. Unaweza pia kuvaa juba au ushungi kufunika nywele zako. Hii itaonyesha wazi imani yako ya dini na kusitiri mwili kulingana na maelekezo ya dini yako. Kama wewe ni mvulana, pengine utapenda suruali, fulana na nywele fupi. Lakini, nani ajuaye, mtindo wako na chaguo lako linaweza kuwa ni kufuga afro au kusokota dreads, au kuwa na mtindo ambao unaashiria kabila lako. Mavazi yanaweza kubeba utambulisho wako.



AFTER

Kumbuka:
Usiogope kujitambulisha kwa mavazi na mtindo wako wa nywele. Jiamini na siku zote thubutu kuonyesha wewe ni nani!



TIRIRIKA
Mavazi na urembo vinakusaidiaje katika kujiamini?

ANITHA TINYA, 17
Maswa, Simiyu



Ninapokuwa nimependeza najihisi nina mwonekano mzuri kisura na kimwili. Hivyo hiyo tu inanifanya nijiamini kwakuwa sina wasiwasi na mwonekano wangu.

GEORGE FIDELIS
MWAKANYAMALE, 16
Tunduma, Songwe



Mimi nimekuwa nikipenda sana kuvaa nguo kwa kufananisha rangi. Hii inanifanya nijihisi naonekana vizuri, hivyo inaniongezea hali ya kujiamini ninapofanya mambo yangu. Unapokuwa hauko nadhifu kila wakati unakuwa na wasiwasi na mwonekano wako, unakosa uhuru hata unapojieleza mbele za watu.

SOPHIA JUSTINE
DAUDI, 15
Mara, Musoma



Mitindo na urembo vinanisaidia kujiamini. Kwa mfano nikivaa nikapendeza, kila ninakopita wananisifia nimependeza, hiyo hali tu inanijenga au inanifanya niweze kujiamini popote niendapo.

Sekela pia anaiweka wazi haiba yake. Hapa anatushirikisha mambo anayoyapenda na asiyoyapenda. Anapenda kuchati, kucheka na kutengeneza marafiki wapya. Anapenda pia kudansi, kuimba na michezo. Lakini pia anapenda kusafiri – kujionea maeneo mapya na kukutana na watu wapya. Haya yote yanachangia namna anavyojitambulisha – anapenda kuvaa nguo za vitenge zenye rangirangi na anaamini zinaendana na haiba yake. Kwakuwa ni mwanamichezo, mara nyingi Sekela si mvaaji sana wa viatu vya mchuchumio. Anapenda mitindo ya nywele, hususan kusukia nywele za bandia na kuremba macho yake kwasababu anapenda yaonekane makubwa. Kwa ujumla, Sekela anafurahia kuvumbua mitindo mipya na kuwa na mwonekano ambao watu watauoanisha na haiba yake.



Kumbuka:
Haiba yako inaweza kujieleza kwa namna unavyovaa na kwa namna unavyoonekana kwa ujumla.

Katika kukua kwake, Sekela amegundua mambo mengi kuhusu namna anavyojisikia anapokuwa na watu wengine. Amegundua kwamba wakati mwingine anajisikia aibu anapokuwa katika kundi la watu wengi, hasa kama siku hiyo hakuzijali nywele zake. Anahitaji kitu fulani kumwongezea uwezo wa kujiamini. Kuvaa vizuri na kutengeneza nywele kunasaidia kumfanya awe na 'mood' nzuri. Anaweza kutembea kifua mbele na anapoingia mahali anajisikia kwamba ni mwenye mvuto na mwenye nguvu. Huo ndio uzuri wa kuwa na uhuru wa kuchagua unataka kuvaa nini na uvaje!

Kumbuka:

Kujiamini na kujitambua ni mambo muhimu katika kila jambo unalolifanya! Hebu chunguza namna mavazi, mitindo ya nywele na vipodozi vinavyoweza kukusaidia. Lakini pia kumbuka kwamba, wewe mwenyewe ndiye unayeamua haiba yako iweje. SI LAZIMA UJIPODOE. Hata kama rafiki zako wote wanajipodoa unaweza kuamua kutokujipodoa kama ndilo chaguo lako. Ujipodoe, usijipodoe, unapendeza tu. Si lazima ufanye jambo eti kwasababu kila mtu anafanya.

Be yourself!

DRESS FOR SUCCESS!

BY FEMA TEAM

We dress, we do our hair, sometimes we put makeup on. The way we 'look', the way we 'style' and present ourselves to the world, tells the story of who we are and what we want to be. Dressing is personal, it is 'art' as we use our bodies as a canvas to communicate.

Who taught you about dressing and expressing your style? Is it something you enjoy? Sekela, our girl power team member, tells us her story.

When I was about ten, I recall waking up in the morning, watching as my mother was getting ready for her day - choosing a dress, tying her hair and sometimes putting 'makeup' on. Her 'style' would change when going to worship, visiting a friend, going to a wedding, or to the market to purchase things for her shop. I was amazed at how different she could make herself look. When she would dress in colorful fashion gowns and put red lipstick on, she was full of confidence and good humor. Other times, when she would wear more respectable dresses she would be more subdued, and yet other days she would dress in black and I would know - mama is sad.

I adored my mother, she influenced me deeply and I understood that dressing is an important key to being a person. I learnt early that the way you present yourself to the world can make a difference. People would react differently to my mother according to the way she dressed and it would make her feel different too. Already as a child I loved to dress up, I had my favorite yellow dress that made me feel happy. When I was in school, I had to use my school uniform and keep my hair short. That was ok, but I longed for the day that I would graduate, when I could dress up and experiment with my hair! I was so eager to express myself and understand who I could be.

This is what Sekela learnt about dressing up:

She learnt about her IDENTITY! What is an identity? Identity is who you are. Are you a boy or a girl? Are you a student? Are you young or old? What community do you belong to? Identity definitely affects how you dress and how you present yourself to the world. Dressing sheds light on who you are, why you make certain dress style choices, and it is a way to better understand others. Feedback on the clothing we wear is also important, our dressing triggers responses in people, you can dress to provoke, to make a statement or to simply disappear. If you are a girl like Sekela, you will probably like skirts and dresses. But let's not get caught in stereotypes, girls may like wearing pants and have more of a unisex look. You might plait your hair, or use extensions and try different styles, or you may wear the hijab scarf and cover all your hair. This speaks clearly about your religious community and what they consider appropriate exposure of the female attributes in public. If you are a boy you will probably like trousers and t-shirts and keep your hair short. But who knows, your style and sense of self may feel like having a long afro or dreads. You may like to wear or do something that communicates your tribal affiliation. Many things about your identity can be reflected in how you dress yourself.

Remember: Don't be afraid to show your identity through your clothes and hair styles. Be confident and always dare to show who you are!

Sekela has also grown to express her PERSONALITY. These are her likes and dislikes. She likes to chat, laugh and make friends. She likes to dance, sing and do sports. She also likes to travel and see new places and meet new people. This all contributes to how Sekela expresses herself - she loves dresses with bold and colorful kitenge patterns and thinks it matches her personality. As an athlete she rarely wears high heels. She loves hair styles, especially extensions and eye makeup, as she wants her eyes to look bigger. All in all, Sekela enjoys finding her own style, and things that people will recognize as being all about 'her' personality.

Remember: Your personality can be expressed with details of dressing up and are also part of how you present yourself.

Sekela has grown to learn a lot about how she feels when she is with others. She has realized that sometimes she feels shy when in large groups, especially if she has a 'bad hair day'. She needs something to boost her CONFIDENCE and her SELF ESTEEM. Dressing up and having her hair done, helps boost her mood! She can then walk with her head high, and when entering a room - feel attractive and powerful. That is the beauty of being able to choose what you wear and how you want to wear it!

Remember: Confidence and a positive self-esteem is important for everything you do! Explore how dressing, hair styling, even make up can help! Wear your confidence with pride! But it is also important to understand that you do not have to wear make up. Even if you are surrounded by people who wear make up, you can still choose to go natural if that is what you like. With or without makeup, you are beautiful. You do not have to do something simply because everyone else is doing it.

Be yourself!




CHATA LA


TIZO


TIZO AKA T KAHITIMU KIDATO CHA SITA, YUPO KITAA. ANAJISEMA KIMOYOMOYO "SASA NIMEKUWA RAIA!" NA KWA JINSI ALIVYOLIELEWA PEPA, ANATARAJIA KUTUSUA KINYAMA! BILA SHAKA ATATINGA CHUO KIKUU. ANA USONGO NA CHUO MPAKA ANAONA SIKU HAZISONGI! JE, ITAKUWAJE? FUATILIA!

MIEZI MITATU BAADA YA KUENZA CHUO



TIZO AKIFANYA KWELI







BOY PLEASE WALK OUT!

IF YOU WANT TO ATTEND MY LECTURE, DRESS DECENTLY AND REMOVE THOSE TATTOOS!



UNOKO TU, MI NSHAKUWA MTU MZIMA BANA



BAADA YA MIAKA MITATU TIZO AKAOMBA KAZI SERIKALINI AKAITWA KWA INTERVIEW



...MASUALA YA LOBBYING, UONGOZI, PROPOSAL WRITING NIKO VIZURI SANA

WIKI MOJA BAADAE



UMECHAGULIWA KATIKA NAFASI YA...

NIKO TAHARI KUANZA HATA SASA



DAAH! NITAVAA PULL NECK NA SUTI MPAKA LINI JAMANI? HIVI HAIFUTIKI HII KWELI?



...AKATINGA TATOO HOUSE

HIVI HUWEZI KUIFUTA HII KITU AISEE!?

KUNA SEHEMU WANAFUTA LAKINI GHARAMA YAKE HUIWEZI



E BWANA EE TIZO LEO SI KATIMULIWA CLASS

UNOKO TU...KUFUATILIANA TU, UTADHANI ANANILIPIA ADA

NINI KWANI!?



MAVAZI ALIYOVA LEO YAMEMCHORESHA TATOO ZAKE

NA ULE MLEGEZO BILA SHAKA

KUNA KISA BASI? UNOKO TU. MAVAZI YANGU YANAMHUSU NINI



TIZO AKISAINI MKATABA

SAINI NA HAPA KWENYE MUONGOZO WA MAADILI

DUH! TATTOO HAZITAKIWI?MMH! NIKANUNUE PULLNECK ZA KUTOSHA KUFICHA HILI CHATA



TIZO AKAANZA KUONJA JOTO YA JIWE

JOTO? HAPANA!

AC YOTE HII JOTO LI TOKE WAPI?

JOTO KALI, AC IKO ON KWELI?



MNAJUA TATOO HAZIRUHUSIWI KWA MTUMISHI WA SERIKALI?

KAMA NDO HIVYO NIMEGHAIRI

DUH! NIRUDISHIE HELA YANGU


OYA TUSIHARIBIANE BIASHARA!



AMA KWELI MAJUTO NI MJUKUU

*PICHA: RAPHAEL NYONI
 *UONGOZAJI: PENDO MASHULANO
 *WAIGIZAJI: TANDALE YOUTH GROUP
 *SHUKRANI: OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA, IDARA YA UKUZAJI MAADILI SERIKALINI

Ni **tattoo** na kadhalika....



Tattoo ni moja ya vitu ambavyo havitakiwi katika mwonekano wa mtumishi wa umma. Hii ni kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa mwaka 2007 na Idara ya Ukuzaji wa Maadili Serikalini iliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Tizo hakujua! Alikuwa ni fan mkubwa wa msanii Whiz Khalifa, alitamani sana mwonekano wake, na kwakuwa ujana maji ya moto, alipopata boom lake tu akajipiga chata moja matata shingoni! Tizo sasa anajuta! Pull neck haimtoki mwilini muda wote wa kazi, iwe joto, iwe baridi, iwe kiangazi, iwe masika! Analinda kibarua!



Chata la Tizo lilikuwa temporary tu.
Yote ni katika kunogesha mchezo.

Sio tattoo peke yake!

Kwa mujibu wa mwongozo wa mwonekano wa mtumishi wa umma, baadhi ya vitu ambavyo haviruhusiwi kwa mtumishi wakati wowote awapo kazini ni:



KWA WANAUUME

- ✗ Nguo ambazo ni za kazi maalum kama vile michezo (Hizi zivaliwe wakati wa shughuli hiyo tu).
- ✗ Nguo ambazo zina michoro, maandishi na picha ambazo haziendani na shughuli za serikali.
- ✗ Nguo zinazobana.
- ✗ Kaptura ya aina yoyote.
- ✗ Suruali yoyote inayoachwa bila kupindwa chini.
- ✗ Suruali za "Jeans" na Fulana "T-shirts" (Hizi zivaliwe tuwakati wa shughuli maalum inayotambulika).
- ✗ Kikoi au msuli.
- ✗ Nguo zenye maandishi ya chama chochote cha siasa na yenye kuonyesha ushabiki wa kitu fulani.
- ✗ Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.
- ✗ Nywele chafu na ambazo hazikutengenezwa vizuri.
- ✗ Nywele zilizosukwa mitindo ya aina yoyote ile.
- ✗ Ndevu zisizotunzwa vizuri.
- ✗ Kandambili.
- ✗ Viatu vya michezo (Labda wakati wa shughuli maalum za michezo).

KWA WANAWAKE

- ✗ Nguo zinazobana.
- ✗ Nguo fupi ambazo zinaacha magoti wazi.
- ✗ Nguo ambazo zinaacha sehemu ya mwili wazi kama vile kitovu na kifua.
- ✗ Nguo ambazo zina picha, michoro na maandishi ambayo hayaendani na shughuli za serikali.
- ✗ Kaptura aina yoyote ile kama vile pedo na pensi.
- ✗ Nguo zinazoonyesha maungo ya mwili (transparent).
- ✗ Suruali za jeans (isipokuwa pale mtumishi wa serikali anapokuwa katika shughuli za nje, yaani field).
- ✗ Suruali yoyote iliyoachwa bila kupindwa chini.
- ✗ Fulana/Tshirts (hizi zivaliwe tu wakati wa shughuli maalum inayotambulika).
- ✗ Nguo ambazo ni za kazi maalum – michezo, kazi za nje au burudani. Hizi zivaliwe mahususi wakati wa utekelezaji wa shughuli hizo.
- ✗ Nguo yenye maandishi ya chama chochote cha siasa au ushabiki wa kitu fulani.
- ✗ Nguo yoyote inayopingana na maadili ya utumishi wa umma.
- ✗ Nywele chafu na ambazo hazikutengenezwa vizuri.
- ✗ Kandambili.
- ✗ Viatu vya michezo (isipokuwa wakati wa shughuli maalum za michezo).
- ✗ Mikufu ya miguuni (vikuku).
- ✗ Kuweka vipini maeneo mbalimbali ya mwili kama puani na sehemu nyingine tofauti na hereni za kawaida.



Lengo ni nini?

Mkurugenzi wa Ukuzaji Maadili Serikalini, Fabian Pokela, anasema, mwongozo huu kwa ujumla wake unasisitiza unadhifu katika mavazi na mwonekano. Lengo ni kulinda heshima ya serikali. "Serikali ina hadhi yake. Lazima hadhi hiyo ilindwe. Uzuri ni kwamba mwongozo huu ni sheria, hivyo mtumishi wa umma anatia saina taratibu hizi wakati anaposaina mkataba wake wa ajira. Hatarajiwi kwenda kinyume".

Pokela anasema, mwongozo huu unawahusu watumishi wa umma, lakini baadhi ya taasisi, kulingana na mazingira ya shughuli zake, wameamua kwamba utawahusu pia wateja wao. "Pengine hii ndiyo sababu umewahi kufika sehemu kama hospitali, shuleni au chuo ukazuiwa kuingia kwasababu hukuwa katika mwonekano sahihi".

USIWE KAMA TIZO!

Wahenga wetu walisema, ujana maji ya moto. Hawakukosea! Kuna mambo tunafanya tukiwa vijana, baadaye tunayajutia. Mbaya zaidi kuna mengine hayarekebishi au yanarekebishi kwa gharama kubwa sana, kama Tizo na tattoo yake. Ujumbe tunaokuacha nao ni kwamba tafakari, chambua faida na hasara za jambo kabla hujalifanya.



Albert alinyanyuka, akaenda kabatini, na kuchukua picha moja hivi. Ilikuwa imefunikwa, bila shaka kwa kuihifadhi katika usalama. Albert alirudi mezani, akaketi, na kisha akaifungua mbele yangu. Hakusema chochote.



Picha ilikuwa kubwa na ilikuwa ya mama wa makamo, aliyesimama nyuma ya uzio. Kwa macho yangu mama huyo alionekana jasiri, lakini pia kama alikuwa amepitia mengi, mazito. Aliitazama lenzi ya kamera bila kusita. Machoni ni kama vile machozi yalimlengalenga, lakini huwezi kujua kwa uhakika. Alionekana mwenye uchungu moyoni, lakini, sikuwa na uhakika na hili pia. Nilitazama hii picha kwa muda mrefu, na ingawa nilikuwa na maswali mengi sana kichwani, nilitamani kujua stori ya mama huyu, sikuwapa majibu.

“Ana stori gani mama huyu?” Niliuliza. “Kabla sijakusimulia stori ya mwanamama huyu, wacha kwanza nikusimulie stori yangu,” alisema.

Hata bila rangi unaweza kupata picha bomba kama hivi.



"Mimi naitwa Albert Mbepera. Nimesoma Shahada ya Anthropolojia ya Utamaduni na Utalii, Chuo Kikuu cha Tumaini. Mimi ni mpigapicha, na kama nikiulizwa mambo matatu ambayo nayapenda sana, kwa hakika nitasema, kupiga picha, kusafiri na kuthubutu kufanya mambo mapya, makubwa. Ndoto yangu ni kwamba ifike siku nipige picha ambayo itakuwa gumzo dunia nzima na natumaini picha hiyo itakuwa imebeba stori ambayo itawafanya watu wote duniani wathamini utu.

Safari yangu katika taaluma ya upigaji picha ilianza chuoni. Katika somo la upigaji picha na pia kutokana na umahiri wa mwalimu wangu wa somo hilo, nilijenga mapenzi makubwa sana na kamera na picha! Nakumbuka, tulikuwa na kamera moja tu ya kufanyia mazoezi, lakini naweza kusema kwamba, mimi ndiye niliyeitumia kuliko wanafunzi wote! Nilikwenda mbali zaidi na kusaka maarifa mtandaoni kuhusu upigaji picha. Vijana wa leo tuna bahati kubwa sana! Unaweza kuzama Youtube ukajifunza mambo kibao kuhusu upigaji picha – na kuna kozi kibao online! Search tu!

Mwaka 2013 nilianzisha kampuni yangu, nikaita Manifester. Jina hili lilitokana na neno 'manifestation' katika Biblia, neno ambalo linamaanisha 'kubainisha/kudhihirisha' vitu. Nisingeweza kufanya yote haya bila mwongozo wa mshauri wangu, Raqey Allaraqya wa I-View Studios. Yeye ndiye 'aliyenipika' nikaiva sawasawa wakati nilipokuwa nikifanya kazi katika kampuni yake kama msanifu wa kurasa (graphic designer) mwaka 2010. Wakati huo filamu za kibongo zilikuwa moto sana na watu wote maarufu walikuwa wakija kwake kupigwa picha! Hivyo, kupitia kwake, nilikutana na watu maarufu! Ilikuwa ni kama ndoto yangu imetimia!

Hakuna anayefanya harusi asitake kumbukumbu. Hii nayo ni kazi ya mikono yangu

Picha za harusi ndiko nilikojikita zaidi



TIRIRIKA

Kwanini vijana wanapenda sana kupiga picha?

HAPPYNES MAGILE SALU (14), SIMIYU

Ni kwa sababu ya utandawazi. Siku hizi kuna simu za mkononi, zina camera, basi kila mtu anaweza kupiga picha. Hata gharama za wanaopiga picha kibiashara zimeshuka, tunazimudu.



HARUN. M. HAYOEL (21), MARA

Tunapenda kupiga picha ili kutunza kumbukumbu ya mahali tulipowahi kuwa, jinsi tulivyowahi kuvaa na watu tuliowahi kukutana nao. Ndio maana mara nyingi nyuma ya picha zetu tunapenda kuandika majina ya waliopo pichani na tarehe ya kupigwa picha. Ni kumbukumbu nzuri.



SAID HUSSEIN (15), GEITA

Vijana wengi wanapiga picha ili kutafuta masoko ya bidhaa zao kupitia mitandao mbalimbali ya kijamii. Mfano kwenye Facebook, Twitter na Instagram ili waweze kujikwama kiuchumi na kujikimu katika maisha ya kila siku.



SMS: Andika FEMA acha nafasi andika maoni yako kisha tuma kwenda 0753 003 001. SMS tu, usipige!



Naamini kwamba mtu yeyote anaweza kuwa mpigapicha. Muhimu ni kuwa na mapenzi na kazi hii. Nikupe siri moja, mshauri wangu, Raqey alitumia kamera ya kawaida kabisa alipoanza kazi hii. Alitumia kompyuta kuhifadhi na kuhariri picha. Lakini kwakuwa alikuwa na mapenzi na kazi yake, nidhamu kazini na malengo, vyote hivyo vilimwezesha kufanikiwa.

Changamoto ziko kibao katika kazi hii ya upigaji picha. Kwanza, watu hawajui thamani ya picha. Ukweli ni kwamba, picha ni kitu kinachodumu maisha yako yote. Kwa mfano, watu wanapokuwa na shughuli, wako tayari kulipa fedha nyingi kwa ajili ya ukumbi au chakula. Lakini, vyote hivi vina-expire kabla hata shughuli yenyewe haijaisha! Lakini, picha zitabaki milele.



Inapendeza sana kuona maisha ya kawaida pichani kama hivi

“Mwanangu, nimekuona ukinipiga picha. Endelea tu, nina mambo makubwa ya kunitia wasiwasi, hilo ni dogo sana. Nilipokuwa shamba leo asubuhi, nafsi yangu ikaniambia kuna jambo haliko sawa nyumbani. Hivyo nikaianza safari ya masaa mawili kwa mguu kurudi nyumbani, ndipo nikakuta binti yangu mdogo niliyemwacha nyumbani, hayupo. Nikawauliza majirani kama wamemwona, ndipo waliponiambia kwamba amekimbizwa hospitali. Kutoka nyumbani kwangu kufika hospitali ni mwendo wa saa sita, na ndio kwanza nimefika hapa hospitali. Sijamwona binti yangu na madaktari hawajaniambia chochote. Kwahiyo, niko hapa, nina wasiwasi kuhusu mwanangu.” Kwa habati mbaya, sikupata fursa ya kujua stori ya huyu mama ilikwishaje.



Kamera inakupa mambo matamu kama hivi, hasa ukijua kucheza nayo.

Pili, kununua vifaa vya kisasa vya picha ni gharama kubwa sana. Unapaswa kuweka akiba ya maana ili upate vifaa sahihi. Na tatu, jamii yetu ina kawaida ya kuthamini zaidi picha za watu maarufu badala ya zile zinazoonyesha uzuri wa nchi yetu na watu wake, picha ambazo pia napenda kupiga. Hakuna soko la picha za namna hii hapa kwetu Tanzania, kama lipo, ni finyu sana. Na hiyo ndiyo sababu kwa sasa nimezama zaidi katika kupiga picha za harusi. Hata hivyo, bado nina imani kwamba kupitia picha za harusi, naweza kudhihirisha ndoto za watu na kuwapa kile ambacho roho zao zilikitamani katika siku yao hiyo maalum.

Sasa, hebu turejee katika ile picha niliyokuonesha mwanzo. Kila picha ina stori yake. Wala sifahamu jina la huyu mama pichani na hata yeye sidhani kama ananifahamu. Nilikutana naye Simiyu, Kaskazini Magharibi mwa Tanzania. Baada ya kumpiga picha, nilimsogelea nikamuuliza kinachomsibu, hivi ndivyo alivyoniambia:



Manifester himself

Naomba niseme kwamba, ushauri wangu kwa vijana na wasomaji wa Fema ni:

- 1 Ipende kazi unayoifanya. Utapata matokeo mazuri kama unachokifanya unakifurahia.
- 2 Soma, tafuta taarifa! Siku zote uwe tayari kujifunza zaidi na zaidi!
- 3 Upigaji picha unalipa. Jitume. Inawezekana!





Albert walked over to a shelf and pulled out a covered photograph that he obviously kept safe. He came back to the table and sat down, then opened the big photo in front of me. He didn't say a word.

The photo showed an elderly woman who stood behind a steel fence. To me she looked strong, and like she had been through a lot. She gazed straight into the camera's lens, without hesitation. Her eyes seemed teary, but one couldn't be sure. She seemed sad, but again, one couldn't say that with certainty. I looked at the picture for a very long time, and though I came up with many questions on what could be the story of this photo, I just couldn't find the answers.

"What's her story?" I asked. "Before I tell you this woman's story," he said, "let me tell you mine."

"My name is Albert Mbepera. I studied Cultural Anthropology and Tourism at Tumaini University. I am a photographer by profession, and if asked the three things that I am most passionate about, then I'd definitely say photography, travelling and taking risks. My dream is to one day take a photograph that will be recognized internationally and I hope this picture will bear a story that will make everyone value humanity.

My journey towards professional photography began in college. Through the photography classes that I took, and interesting teacher that I had, I developed a strong passion for taking pictures. I recall that we only had one camera to practice, but I can tell you, I was the one who practiced the most! I also went on to research more about photography on the internet. The youth today are so lucky! You can learn photography on Youtube and through many free online courses! Just search!

I founded my company, Manifester Brand, in 2013. The name was inspired by the word 'manifestation' in the Bible, which meant to 'manifest' things. I couldn't have done it without my mentor, Raqey Allaraqya of I-View Studios. He was the one who coached me while I worked at his firm as a graphic designer in 2010. At that time, Bongo films were very popular and all the famous people used to have their photos taken by him! So, through him, I also met them! It was such a dream come true!


I believe that anyone can be a photographer. What is most important is that one has the determination and the passion. Here's a secret, my mentor Raqey used a normal camera and a computer when he started, to be able to take, collect and edit the photos. But it was his passion, work ethic and the determination, that made him succeed.

The challenges in photography are many. Firstly, people do not realize the value of photography, but the truth is, pictures last a lifetime. For example, at an event, people will pay more money to hire a venue or pay for food. And all these expire before the day ends. But photographs last forever. Secondly, purchasing the right equipment is not cheap. One needs to save so as to invest in the right gear. And thirdly, the public tend to value photos of celebrities and famous people, instead of pictures that show the beauty of nature, the country and its people which I love to capture. There is little to no market for such images here in Tanzania. That is why I currently do mostly wedding photography and not nature photography. However, it is still my hope that through wedding photography, I can still manifest people's dreams and make their wishes for their special day come true.

Now back to the photograph I showed you in the beginning. Every image has a story behind it. I don't know her name of the woman in the picture and I doubt that she knows mine. I met her in Simiyu District, North West of Tanzania. After taking the pictures, I walked over and asked her about her story, and this is what she told me:

"My son, I saw you taking pictures of me. Go ahead as that is the least of my worries. As I was working in the fields this morning, my intuition told me that something was not well at home. So I walked the long two hour walk back home, only to find that my young daughter, whom I left at home, was not there. I asked the neighbors if they had seen her and they told me she had been rushed to hospital. It's a six hour walk from my house to the hospital, and I have only just arrived. I have not seen my daughter yet and the doctors have not told me anything. So, I am here, worried about my child." Sadly, I did not get a chance to find out how the lady's story ended.


- Needless to say, my advice to youth and Fema readers is:
- 🎯 Be passionate and love what you do. The best work comes when you enjoy it.
 - 🎯 Read and research! Always be willing to learn more and more!
 - 🎯 Photography can earn you an income. You just need to be dedicated. It can be done!



TANZANIA YA SANAA

Sanaa na ufundi ni moja ya nguzo muhimu sana katika utamaduni wa Mtanzania. Nyanja hii hugusa moja kwa moja maisha ya kila siku ya Mtanzania, kijamii, kihisia na hata kiuchumi. Hebu tuone kazi mbalimbali za sanaa zinazofanyika nchini kwetu.

11 SUSTAINABLE CITIES AND COMMUNITIES



Vyungu vya maua

Hakuna barabara utakayopita bila kukutana na vyungu mwanana vitakavyoburudisha macho yako, vyungu vizuri kabisa vya kuweka bustanini na kupendezesha mandhari. Hapa mimi naona maua vyungu na fursa. Sijui wewe mwenzangu unaona nini?



Mapambo ya Shanga

Badala ya kuvaa hereni za chuma, shaba, au english gold wadada siku wanapendelea zaidi kutokea kiasili, si unacheki mwenyewe hapo mapigo ya kila namna!?



Ungo kutoka Mbeya

Jiko ni moja ya sehemu ambazo sanaa ya upishi huchukua hatua, na katika maandalizi ya chakula mara nyingi ungo huchukua nafasi kubwa sana. Wataalamu wazuri wa kupamba nyungo katika Tanzania hii hupatikana Jijini Mbeya, na ndio maana nyungo za Mbeya hupendelewa zaidi kwa ajili ya uzuri na ubora wake.



Sandals za kimasai

Wamaasai wanasifika sana kwa kudumisha utamaduni wao, lakini inawezekana pia kipo cha ziada cha kuwasifia ambacho ni uwezo wao wa kutengeneza viatu vya wazi vinavyopendwa sana. Hivi nani hajawahi kuvaa sandals za kimasai? Siku hizi zimekuwa tamu zaidi hasa kwa

manjonjo ya hapa na pale. Vinanogaje!?



Utengenezaji wa Batiki


Batiki! Hivi ni nani asiyependeza ndani ya vazi la Batiki? Ni fursa nzuri sana ya kibiashara na sanaa hii haichagui eneo. Ni rahisi kujifunza na kutengeneza Batiki. Unaweza ukapika na kuuza kama majora au ukashona na kuuza nguo za batiki na kupiga mkwanja.

Ubunifu wa bustani

Wanasema uzuri wa nyumba ni choo lakini hapohapo ongeza na mandhari ya kuvutia. Siku hizi maua imekuwa ni ajira ya vijana. Wanaremba bustani za biashara na hata za nyumbani. Hapa ni mji mwema Garden ndani ya Kigamboni.

Uchoraji na Uchongaji

Hizi sanaa ni adhimu sana. Kwanza zinahitaji muda, uvumilivu na ubunifu wa hali ya juu, bila kusahau elimu. Zamani tuliaminishwa kwamba sanaa zinarithishwa kutoka kizazi hata kizazi lakini ukweli ni kwamba unaweza kwenda shule na ukajifunza. Kipo Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TASUBA) ambacho kinatambulika kwa kupika wanataaluma katika nyanja hii.



Vikapu toka Iringa

Umaarufu wa vikapu sio jikoni tu. Siku hizi vinatumika hata chumbani. Ndio! baadhi ya watu wanatumia kuwekea nguo chafu. Ukitaka vikapu vya ukweli unajua vinatoka wapi? Kila mkoa una style yake ya vikapu ila vikapu vya Iringa vitabaki kuwa juu!

MAF

ARUSHA

SINGIDA

DODOMA

IRINGA

TANGA

LIN

DUMUMA

MPENDWA ANTI



Iwapo una tatizo lolote kuhusu mabadiliko ya mwili wako, afya yako, matatizo ya kifamilia, shule na hata marafiki tafadhali tuma kwa Mpendwa Anti:

FEMA


S.L.P. 2065, Dar es Salaam

e-mail: info@femahip.or.tz

SMS: 0753003001

Mimi naitwa Yohana Tungu kutoka Igunga, Tabora. Nimeoa na nina miaka 22. Swali langu ni kwamba Anti Fema, mwanamke akipata ujauzito huwa siku zake za hedhi zinaendelea au inakuwaje?

◆ Habari? Kwa kawaida mwanamke akipata ujauzito, hatapata tena hedhi hadi atakapojifungua. Ni muhimu pia kuzingatia kwamba wanawake wanatofautiana, na hivyo, wachache, hasa wanaonyonyesha ipasavyo hawapati tena hedhi hadi atakapoachisha mtoto kunyonya. Jambo muhimu zaidi ni kwamba kila mwanamke mjamzito anapopata hedhi, afike hospitalini apate ushauri wa daktari.



Mpendwa Anti. Nifanye nini ili harufu ya mdomo iishe? Pia meno yawe meupe? By Salha.

◆ Habari. Harufu ya mdomoni inaweza kusababishwa na magonjwa ya fizi na meno. Kama kinywa hakitosafishwa vizuri, au mabaki ya chakula yasipoondolewa vizuri inaweza kusababisha bakteria kuzaliana kwenye kinywa huku wakiozesha mabaki ya chakula na kuharibu fizi. Baadhi ya vyakula pia husababisha harufu mbaya mdomoni hasa mabaki ya nyama kwenye meno na vile vyenye sukari. Harufu pia inaweza kusababishwa na matatizo kwenye mfumo wa chakula, hasa kuzidi kwa nyongo tumboni. Kupunguza harufu mdomoni ni vema kufika hospitali kwanza kwa mtaalam wa afya ya kinywa ili ujue tatizo lako linasababishwa na nini, kisha fuata ushauri wa daktari ili kupata suluhisho la kudumu. Daktari pia atakupa ushauri wa namna ya kufanya ili meno yako yawe meupe zaidi huku ukiyalinda. Pia ni vema kusafisha kinywa angalau mara mbili kwa siku na ikibidi mara baada ya kula vyakula vyenye harufu kali. Punguza ulaji wa vyakula vyenye sukari pia. Jitahidi kunywa maji mara kwa mara ili kupunguza uzalishaji wa bakteria kinywani kwani maji yanapopita kwenye kinywa yanasafisha ulimi na kinywa pia.


Naitwa James, nasoma kidato cha tatu. Ninaishi Mwanza. Tafadhali naomba kuuliza, hivi kama wazazi wakikataa kukusomesha na wana uwezo, na pia unafaulu vizuri darasani unatakiwa ufanyaje?

◆ Habari? Kwanza ongea na wazazi ili waelewe kwamba ungependa kuendelea na masomo yako. Pia unaweza kuomba mwalimu wako afike nyumbani kuongea na wazazi ili waelewe na wakusaidie kufikia malengo yako. Mwalimu wako pia anaweza kukusaidia zaidi kuona kama kuna haja ya kuutaarifu uongozi wa kata na wilaya kama mazungumzo ya awali yatagonga mwamba. Elimu ni haki ya kisheria ya kila mtoto/kijana na wazazi wana wajibu wa kuhakikisha watoto wao wanapata mahitaji muhimu, ikiwemo haki ya kupata elimu.




Naitwa Yassin Ong'o from Chikonji Lindi. Nimemaliza kidato cha nne 2018, na ndoto zangu ni kuwa polisi na wala sihitaji kuendelea na kidato cha tano. Je, nifanyeje ili nitimize ndoto zangu, nisaidie Anti.

◆ Habari za Chikonji Yassin? Hongera sana kwa kujua unahitaji nini. Ningependa ufahamu kuwa jeshi la polisi linahitaji wataalam wa fani mbalimbali, kuanzia wanasheria, wahasisibu, walimu, wahandisi, watu wa ustawi wa jamii na wengineo. Hivyo utakuwa na msaada mkubwa zaidi kwa jeshi hilo endapo utaendelea na masomo yako. Ukiendelea kidato cha tano itafaa zaidi, na ikishindikana basi hakikisha unajiunga na chuo na upate angalau diploma, ili uwe na nafasi nzuri zaidi kwani sasa jeshi linaajiri zaidi wale wenye fani/utaalamu mbalimbali.



ANTI COS ANAJIBU MASWALI YENU



Mpendwa Anti, mimi ni mwanafunzi wa kidato cha tano, tatizo langu ni kwamba huwa nakosa confidence ya kuongea mbele ya kadamnasi. Yani huwa natetemeka, mapigo ya moyo yanaongezeka, hata maneno ya kusema nakosa. Je, unaisaidiaje Anti, kwani napenda kuwa na confidence.


◆ Habari? Kwanza ningependa ujue kwamba hauko peke yako, wapo wengi wengine ambao hukumbwa na hali hii. Anza taratibu, kwa kuongelea vitu unavyovifahamu zaidi, hii itakuongezea confidence ya kile utakachokwenda kuongea, mbele ya wengine. Mbinu nyingine ni kwamba unapokuwa mbele ya watu wengi jitahidi usimwangelie mtu mmoja, kama ni umati umeketi au umesimama mbele yako angalia juu ya vichwa vya watu, kwa kawaida hii huonekana kama unamwangelia mtu. Pia, fanya mazoezi zaidi ya kuongea, jiangalie kwenye kioo na ujisikilize unaongea. Pia jaribu, kuongea kila upatapo nafasi, jaribu bila kuchoka, kwani usipochukua hatua na kuanza, hautapunguza woga wako. Ukishapata uzoefu, utajenga confidence ya kuwaangalia watu kwenye macho.

Habari. Mimi ni Mssa Masai wa Morogoro. Nami napenda niwe mwigizaji lakini je mtanisaidiaje?

◆ Habari ni nzuri. Ili kuwa mwigizaji jiunge na kikundi vya sanaa kilichoko kwenye eneo lako na upate nafasi ya kufanya mazoezi kukuza kipaji chako. Ukipata nafasi ya kushiriki kwenye maigizo kwenye hadhira yoyote jitolee kuigiza na unaweza kutoka kwa njia hiyo. Unaweza pia kurekodi video ndogondogo ukiwa unaigiza na kutuma kwa waigizaji maarufu na watengenezaji wa movie pia. Kama hakuna kikundi kianzisha, waalike rafiki zako au vijana wengine mjiunge pamoja. Kumbuka, usitake kukimbia kabla hujatambaa, nenda hatua kwa hatua. Good luck!

Mimi ni mwana Fema Club na ninasoma shule inaitwa Mugumu Sekondari. Nina swali moja hivi, je unaweza ukaacha mapenzi ukaendelea kukaa bila kufanya mapenzi kwa mwaka mzima?

◆ Habari za Mugumu? Ni kweli kabisa, unaweza kuamua kutofanya ngono kwa muda utakaona unafaa, hasa kipindi uko shuleni, ili upate nafasi nzuri ya kufuatilia ndoto zako. Wapo vijana wengi ambao huanza kufanya ngono kwa kudhani kwamba kusubiri ni ushamba, au kwa sababu rafiki zao wanaambia wao wameshaanza. Isikutishe, kila mmoja wetu ni wa kipekee, anakua kwa hatua zake, na ana uwezo wa kufanya maamuzi ambayo si lazima yafanane na ya wenzake. Hakuna madhara unapoamua kusubiri kwanza, badala yake ziko faida nyingi tu, hasa kwa mwanafunzi, kuacha ngono kutakupa wasaa wa kuweka nguvu zaidi kwenye masomo yako. Utaepuka maambukizi ya magonjwa ya ngono, pia kutakuepusha kupata mimba au kusababisha mimba zisizotarajiwa. Unaweza kabisa kusubiri!



Mambo mpendwa Anti, pole na majukumu ya hapa na pale. Swali langu ni kwamba, inaweza tokea kwa msichana asipate hedhi kwa miezi sita? Mimi naitwa Recho.

◆ Habari Recho? Inawezekana kabisa, hasa kwa wasichana ambao ndio wameanza kupata hedhi. Hii ni kutokana na homoni zake kutokaa sawa, pia wasichana wanaobadilisha mazingira, hasa wale wanaokwenda shule za bweni, huweza pia kukosa hedhi kwa kipindi kirefu. Tatizo hili halipaswi kudumu kwa muda mrefu sana, wengine baada ya mwaka mmoja litakuwa limekwisha. Iwapo suala hili litaendelea, basi muone daktari kwa ushauri zaidi.

Habari mpendwa Anti. Naitwa George, mwanafunzi wa Namihoro sec. Je, mwanaume anayepiga punyeto mara tano kwa siku anapata matatizo yoyote?

◆ Habari. Kama mtu anapiga punyeto zaidi ya mara tano kwa siku, au hata kila siku, ndiyo anaweza kupata matatizo. Kwanza ni vema kujuliza kwa nini anapiga punyeto kwa kiasi hicho? Maana, kila kijana, awe mwanamke au mwanaume amepewa uwezo wa kuhimili tamaa za mwili na kutawala hisia zake. Athari ni nyingi lakini kwanza, anaweza kuleta uharibifu kwenye via vya uzazi hasa endapo anatomia nguvu sana. Pili, atajitenga na wengine maana ni lazima uwe faragha kupiga punyeto hivyo kuna uwezekano wa kushindwa kushirikiana vema na wengine. Pia, muda wa kupiga punyeto ni muda ambao angeweza kuwa anafanya vitu vingine. Unaweza kutawala hisia zako na kuacha punyeto.





Ukinibamba class natema nondo, utafurahia unachokiona! Pengine utasema – hivi ndivyo mwalimu anavyopaswa kuwa. Lakini pia ukunikuta viwanja nasherehesha, utasema, 'naam! huyu ndiye MC wa ukwee!'

Ninapokuwa Sengerema Sekondari Jijini Mwanza nafahamika kwa jina la Baraka Bihurugu, mwalimu wa Historia na Kiswahili kwa A level. Lakini niwapo katika kumbi za sherehe, nafahamika kama MC B Capital! Nina miaka 34, nilizaliwa Dar es Salaam, si Mzaramo wala Mndengereko bali ni Muha kutoka Kigoma.

If you find me in class, you will like what you see. You will probably say - this is what a teacher should be like. Then if you find me entertaining the audience at an event you will probably say 'this MC is the real deal!'

At Sengerema Sec in Mwanza I am known as Baraka Bihurugu, the History and Kiswahili teacher for A level students. But in halls of weddings and other events they call me MC B Capital! I am 34 years old and was born in Dar es Salaam, I am neither a Zaramo nor a Ndegereko but rather a Ha from Kigoma.



Sitaisahau 2009.

Ndio mwaka nilioanza safari yangu ya ushereheshaji (MC). Ilikuwa ni katika mahafali ya kidato cha nne shuleni kwetu. Mkuu wa shule akaniteua niwe 'Msema Chochote' siku hiyo, na kulikuwa na umati wa kufa mtu! Sikujivunga. Nilipiga moyo konde, nikakamata mic, nikafanya yangu na kwakweli niliwasha moto!

Ikawa nimegundua kipaji! Na watu wakanigundua. Sikurudi nyuma! Tangu siku hiyo nikaanza kupewa shavu kwenye shughuli mbalimbali kila kona ya Sengerema na hivi sasa mimi ni MC maarufu sana pande hizi. Natengeneza mshiko kwa shughuli hii ya ziada lakini bado nafurahia kazi yangu ya msingi - ualimu!

2009, a year I will never forget.

This is the year I started my MC journey. During form Four graduations at my school, the headmaster selected me to be the MC of the day, and what a crowd it was! I pulled myself together, took the mic, got the event lit up and spirits lifted.

It was a moment of discovery! The talent in me was released and discovered and there was no going back. Thereafter, I started getting calls for events all over Sengerema and now I am a pretty popular MC out here. I make money from this side job but I still enjoy my main job - teaching!



B Capital, ni wa kipekee.

Nina pamba zangu kali! Tena za kutosha; namaanisha suti matata kabisa! Nazipangilia kulingana na tukio. Kuna mambo yanayonitofautisha na ma MC wengine, kwa mfano, siwezi kuvaa nguo moja tu kuanzia mwanzo hadi mwisho wa sherehe; lazima nitabadilisha mida fulani hivi; Pili, huwa natoa zawadi kwa waalikwa; nakwangua vocha, nasoma namba fasta, anayewahi kuingiza hizo namba kwenye simu yake anakuwa amejishindia vocha. Tatu, huwa nawapatia maharusi zawadi - ni picha ambayo nimepozi pamoja nao. Naiweka kwenye frame tamu, naipamba kwa ujumbe mzuri, nawapatia. Ni kumbukumbu ya siku yao maalum.

Ninapokuwa nasherehesha huwa sizungumzi sana. Ni mtu wa maneno machache. Natoa muda wa kutosha kwa watu kusakata muziki na kufurahi. Mimi pia ni dancer mkali! Naunga tela, nasakata muziki. Haya yote yanarifanya kuwa tofauti na ma MC wengine.

I am unique.

I have many beautiful attires; suits to be specific, and I wear them according to the event. There are certain things that make me stand out, like I don't wear the same clothes from the beginning to the end; I change. Second, I give out goodies to the guests: I scratch phone cards, read them out and the fastest fingers in the room gets airtime. Thirdly, I give out free pictures to the bride and groom. I take a picture with them, frame it with a nice message and hand it to them, to remind them of the day. At ceremonies, I do not speak too much so that guests get time to dance and enjoy the event. I personally am a very good dancer so I join in. All this makes me different from other MCs.





Unafikiria kuwa MC?

Ni kazi nzuri sana tu, inalipa, kama ukijenga jina. Ni sanaa, ni kipaji na si kila mtu anazaliwa na kipaji hiki, lakini niseme pia kwamba, ni kazi ambayo unaweza kujifunza na ukaimudu.

Uzuri wa kazi hii ni kwamba mtaji ni WEWE mwenyewe. Ni kipaji chako na nidhamu ya kazi. Heshimu watu wanaokupa kazi, usiwe na tamaa ukapokea kazi nyingi zikagongana. Wasikilize wateja wako, lakini kubwa kuliko, jali muda. Mengine ni ubunifu wako na kujiongeza. Ukitaka kuongeza thamani yako, weka akiba taratibu, nunua muziki wa maana – si unajua siku hizi watu wanataka MC ambaye atakuja na muziki wake na DJ. Hii itakufanya uwe na soko zaidi na pia itakuongezea kipato.

Planning to be an MC?

Being a MC is a really good job, it pays well if you invest in building your name. It is an art, it is a talent and not everybody is born with it but I must say it can also be learnt.

The good thing about this job is that the capital is - YOU. It is embedded in your talent and professionalism. Respect people's orders for scheduled work, don't get greedy and book too many jobs at the same time. Listen to your clients, but most of all be punctual. The rest is all up to your creativity. If you want to add value, save some capital and buy a good sound system, you see nowadays people want an MC who brings their own music and DJ. That will put you in more demand but also gets you more income.

Changamoto zipo, lakini tucheke!

Kuwa MC sio mteremko. Kuna changamoto zake pia. Basi bwana, siku moja nilipewa kazi ya kusherehesha katika send-off huko Magu. Nikasafiri hadi Magu, kufika ukumbini nakuta kuna MC mwingine anapiga kazi! Nilichoka! Nilikuwa nimepewa kazi na bi harusi mtarajiwa lakini hakujua kwamba familia nayo ilifanya mpango ikatafuta MC. Ila, ndo hivyo, kila kazi ina changamoto zake. Wakati mwingine unapewa nusu ya malipo, wakishamaliza harusi wanakutosa, hawakulipi nusu iliyosalia! Wakati mwingine wageni wanachelewa kufika, shughuli inaanza kwa kuchelewa, basi unalazimika kukimbiza ratiba, inakula kwako, maana unaonekana kama vile hukuwa umejipanga.

Challenges, to laugh at!

Being an MC also has its ups and downs. So, one day I was given a job at a send-off party in Magu. I travelled out there, got to the hall and found another MC in action! I was contracted by the bride and she wasn't aware that the family had hired another MC! It was awful! Of course, every job has its own challenges. Sometimes they pay you less than agreed, sometimes the guests are not punctual, so the event starts late and you find yourself rushing through the program making your job look a bit disorganized. You just have to manage.

Kazi zangu zinapigana tafu

Kuwa mwalimu kumenifanya niaminike, niwe muadilifu na mchapakazi lakini pia kunaisaidia kupata kazi za u-MC kwa urahisi kwasababu watu wanajua mahali pa kunipata. Kuwa MC kunaisaidia pia katika kazi yangu ya kufundisha kwani nakuwa mwalimu rafiki, natoa elimu katika namna inayoburudisha, jambo ambalo linawavuta wanafunzi na kuwasaidia kuelewa somo kwa urahisi.


Nawezaje ku-balance kazi zote mbili? Ni rahisi sana. Ratiba ya masomo huwa ni mchana na shughuli za MC mara nyingi ni usiku, tena hasa wikiendi. Hivyo nina muda wa kutosha kufanya yote mawili.

My jobs complement each other

Being a teacher has made me trustworthy, ethical and hardworking but also a lot more accessible as people now know where they can find me.

Being an MC helps me as a teacher because I get more and more entertaining in class, which gets the students more attentive and active which in turn allows them to understand better.

How do I balance the two?
Very easy. Teaching happens during the day while being an MC happens at night, and mostly weekends. So, I have time for both.



Kuna faida kibao


Sikosi kazi! Nasherehesha katika shughuli ya aina yoyote iwe send off, bag party, harusi na hata sherehe za kidini. Nasherehesha pia katika sherehe za kuvishana pete ya uchumba na hata katika mahafali. Niko bize hatari! Kuwa MC kunaniwezesha kukutana na watu wengi, na kama unavyojua, watu ni mtaji mkubwa sana.

Namudu kuwasomesha watoto wangu na pia namlipia mdogo wangu ada ya chuo. Nina nyumba Mwanza na kiwanja Dar. Nina gari ambalo linarahisisha safari zangu za kikazi na linaniwezesha kufurahia hobby yangu kubwa sana – kutalii katika maeneo ya kihistoria na yenye vivutio.

Wakati nakua...

Ndoto yangu ilikuwa niwe mfanyabiashara mkubwa sana; sijakata tamaa. Tena, nimeshaanza kuifanyia kazi ndoto hii. Nina duka la nguo za kike na za watoto, nafuga kuku na bata na nina bodaboda ambayo nayo inaniingizia senti mbili-tatu.

Najua iko siku nitaanzisha kampuni yangu, nitaaiita B Capital, itakuwa inatoa huduma zinazoendana na kazi ya MC; muziki, video, mapambo na kuuza nguo za maharusi. Nataka kutengeneza ajira kwa vijana wenzangu na najua hili liko mbioni kutokea.



Kabla sijakuaga, lazima niseme hili...

Mimi ni mlezi wa Fema Club shuleni kwetu na hii imenisaidia kuwa MC bora zaidi na imeniongezea umaarufu. Napata michongo ya kusherehesha katika shughuli za Fema Clubs na naomba nimshukuru Kahwa Mpunami, wa Misungwi Fema Club, kwa niaba ya wengine wote kwani huwa ananipa shavu sana na kuniweka bize hapa mjini!

Ushauri wangu kwako msomaji: Jiongeze, jitume, fanya zaidi. Kuwa mbunifu, tambua fursa za kutengeneza mshiko kupitia mambo mbalimbali, ikiwemo sekta hii ya sanaa na ubunifu!

Cheers!



There are many benefits

I am never idle. I MC anything, from send offs to bag parties to weddings and religious events. I do engagement parties and graduations. Being an MC allows me to network with many people and this is a great asset.

Now I am able to not only take my kids to school but also pay for my younger sister's college tuition fee. I have a house in Mwanza and a plot in Dar. I have a car which facilitates my movements and allows me to do what I love the most – touring historical sites.

While growing up...

I wanted to be a big businessman and I haven't given up on that. I have actually started working on it. I have a boutique for women and children's clothes, a poultry farm and a bodaboda that brings in more money.

I know one day I will start my own company that I will call B Capital, which will be MC related, music, video recording, design/décor and selling wedding clothes. I want to create employment for other young people and I believe this will happen.

Before we go, I must say...

I am a Fema Club mentor in our school and this has allowed me to be a better MC and has increased my popularity. I get MC jobs for Fema Club events and I have to thank Kahwa Mpunami, from Misungwi Fema Club on behalf of everyone else because he always keeps me busy.

My advice to all is, always do more. Let's get creative and identify opportunities to earn income through arts and performance.

Cheers!

Hapa ndo ule uwanja wetu wa kujidai! Tunawasiliana na kupiga mastori kibao kuhusu Fema na mambo yetu ya vijana. Kama una chochote cha kusema, huu ndo ukumbi wako mtu wangu. Usisite kutuandikia kupitia sms no. 0753003001, barua kwa S.L.P 2065 Dar, na tovuti yetu ya www.feminahip.or.tz, au hata kwenye page yetu ya Facebook, Instagram na Twitter @Femina Hip. Cheki wenzako walivyofunguka utam hapa chini!

Shairi

Shairi hili limetungwa na
Mwl. Adam Matimbwa.
Shule ya Sekondari Mnero,
Nachingwea – Lindi

- 1 Pongezi zipokeeni, Enyi walezi wa Fema,
Pongezi toka moyoni, Kiukweli ninasema,
Magazeti, redioni, Pote inabamba Fema,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 2 Jitihada mnafanya, Elimu kuisambaza,
Majarida kutawanya, husomwa hadi kusaza,
Ajenda mnazofanya, Taifani kusambaza,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 3 Elimu ya ukatili, wa kijinsia sikia,
Nasi sote twakubali, Jamii kuwafikia,
Mliusema ukweli, uovu kuukemea,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 4 Kwa mimba za utotoni, Tega sikio sikia,
Hivi kweli hamuoni, Jamii mezingatia,
Hapahitaji miwani, ukweli kuutambua,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 5 Hamkuwa na muhali, Kwa ruka juu ajenda,
Kwa ujasiriamali, Hilo nalo mlitenda,
Mmewekeza kwa kweli, Kwa ajenda sema tenda,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 6 Mkurugenzi Minou, Hongera yako ya kweli,
Ama kweli upo juu, Kama Nashi wa Moleli,
umeonesha ukuu, upo imara kwa kweli,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- 7 Amabilis Batamula, Kwa kweli wewe ni noma,
Upo macho hujalala, Kama Glori Mkoloma,
Zauja, Jeni, Sekela, Imara mmesimama,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.

- 8 Dada Pendo Mashulano, Asiyekujua nani?
Wewe kweli ni mfano, Zaidi ya kaka Dani,
Tunaziunga mkono, Juhudi zako jamani,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 9 Kwa nyingi zenu pilika, Nasi pia twaziona,
Hongera sista Rebeka, Nawe Mage wa Maina,
Ujumbe umewafika, Fema ipo kila kona,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 10 Majina nikirudia, wenda sifa nikanyimwa,
Hongera dada Lidia, Nawe binti wa Mginwa,
Dada Asha nae pia, Kwayo maneno kusemwa,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 11 Ukweli unaakisi, Wala hakuna ubishi,
Sifa kwa ka' Matiasi, Nawe pia Bwana Ishi,
Hamna hila ya fisi, Tena hambabaishi,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 12 Sasa natamani kiti, Popote pale kilipo,
Makofi kwake Thabiti, Na ndugu jei Alipo,
Pia na dada Bahati, Kwa mlipo nasi tupo,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 13 Wengine nisiwakose, Popote pale mlipo,
Da'Matha pacha wa Jose, Punga mikono mlipo,
Mwakani tusiwakose, Tembeleeni tulipo,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 14 Nimefika tamatini, Nilitaka kusahau,
Wapi mchora katuni, Si mwingine Baba Tau,
usin'chore gazetini, Kisa nilikusahau,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
 - 15 Koo limenikauka, Kuimba naona kero,
Nisije nikaanguka, Mwisho mkatupwa sero,
Ni Nachingwea natoka, Shule yangu ni Mnero,
Hongereni viongozi, Kwa kazi mnazofanya.
- Adam – umetisha kinyamaaaa!

**HAWA
WAMELONGA
NASI KWA**

SMS

0753003001



Salamu za pongezi kwa Femina Hip. Jumuiya ya Shule ya Sekondari Selebu inapenda kuwapongeza Femina Hip kwa kutimiza miaka 20 ya uelimishaji wa jamii na vijana kwa ujumla. Tumefurahia uwepo wenu, mdumu milele. Big up sana Femina. By Selebu Sec. Fema Club, Kilolo Iringa.

Hello Selebu Sec, tumepokea na kufurahia salamu za pongezi kutoka kwenu. Nasi pia tuwapongeze kwa kuwa moja ya Fema Cub active sana. Sisi sote ni familia ya Femina Hip. We are one big family!!

Hellow Fema magazine, pongezi kwenu kwa majukumu mbalimbali kwa sababu mnatusaidia sana katika mambo tofauti ikiwemo afya, mazingira na jinsi ya kuendesha maisha yetu. Hollah!! by Lissa Charles Elly form 6 EGM, Lupa Sec, Njombe

Pongezi kwako pia kwa kujifunza vitu kutoka kwetu. Tunafurahi sana vijana wanapojifunza vitu vipya kila siku kutoka kwetu na hilo ndilo jukumu letu. Washirikishe na vijana wenzio elimu hii, utatisha sana.

Pongezi kwenu kwa kuchapisha machapisho yenu katika mitandao ya kijamii, najifunza mengi na yananihamasisha kuwa mwanaharakati wa kupigania haki za watoto hasa wa kike. By Zengo Tangawizi toka Mpanda Katavi.

Big up sana kwako Zengo kwa kutumia mitandao ya kijamii kujifunza, na kutaka kuwa mwanaharakati wa haki za watoto wa kike. Usisahau kuelimisha vijana wenzio kutumia mitandao ya kijamii kwa manufaa yao. Wasalimie Katavi.

Habari za kazi Fema magazine, mimi ni Jasmine Mtanda kutoka Ruangwa, natamani nipate majarida ya Fema ila nashindwa. Mnaweza kunisaidia jinsi ya kapata majarida ya Fema? Ahsante, natumai nitajibiwa.

Hi Jasmine, Habari za Ruangwa? Unaweza kujipatia jarida la Fema kwa kupitia mtandao. Ingia kwenye tovuti yetu www.feminahip.or.tz utakuta machapicho mbalimbali ya Fema. Unaweza ukalipakua (download) jarida pia ukipenda. Technolojia imefanya maisha yawe rahisi sana.

facebook @feminahip

Atufigwege Mwajjande

Piga ua garagaza, Femina Hip hamna mpinzani. Nitumie fursa hii kuwapongeza na kuwashukuru uongozi wa Fema kwa kazi nzuri mnayoifanya, safi Sana, Barikiwa.

Nelson M. John

Femina Hip is a good shield to youth in which it prevents us from risk behaviors and bad lifestyles.

Criss Cj

Femina Hip can simply be portrayed as a tool for shaping youth in a proper ideology in terms of Sexual Health, Economic Empowerment and Self Awareness.

Kaiza Ilomo

Tangu niko shule ya msingi hadi sasa chuo kikuu nakubali kazi zenu Femina Hip. Heko kwenu #20yakibabe

MUULIZE ANKO PESA!



Una maswali lukuki kichwani mwako? Unataka kuwa mjasiriamali lakini hujui pa kuanzia? Unaogopa kujitosa katika biashara? Biashara inakwenda mrama? Una senti mbili-tatu lakini hujui uwekeze wapi? Una maswali kedekede kuhusu mambo ya mshiko? USITAABIKE! Uliza ujibiwe na ANKO PESA, mtaalamu wetu wa masuala ya ujasiriamali! (angalia mawasiliano ukurasa wa mwisho wa jarida).



Shikamoo Anko Pesa. Naomba msaada au ushauri kutoka kwako. Kila nikijajiriwa napata shoti, hii sasa ni mara ya 3. Anko Pesa unanishaurije? Niachane na kazi za kuajiriwa?

Naomba nianze kwa kukupa pole. Waswahili wanasema mali bila daftari huisha bila habari. Ni vyema kila unapofanya mauzo ukaandika bidhaa uliyouza na kiasi cha pesa. Na kila aina ya matumizi yanayofanyika wakati ukiwa katika eneo la biashara ni vyema kutunza kumbukumbu ili iwe rahisi kwako kukumbuka wakati wa kufunga hesabu. Tunza kumbukumbu hata ya matumizi ya shilingi mia. Ni vizuri sana kujijajiri, lakini sikushauri uachane na kazi za kuajiriwa kabla hujatatua hilo tatizo la kupata shoti, kwa sababu bila kulipatia ufumbuzi, hata ukijajiri litaendelea.



Shikamoo Anko Pesa na pole kwa kazi. Naitwa Meina, niko Mtwara kidato cha 3. Nina kipaji kikubwa cha utungaji wa simulizi na tamthilia (love stories) na mpaka sasa nina tamthilia 5 ambazo nimetunga lakini nashindwa pa kuanzia. Sina mtu wa kunisapoti wala sijui nitaanzeje kusambaza. Naomba nisaidie nifanyeje?

Habari za Mtwara Meina? Kuna usemi kwamba “ndege mmoja aliye mkononi ni bora kuliko wawili walio porini.” Msanii mkubwa kama Saida Karoli alianza kuimba kwenye vi-send-off na sherehe ndogondogo kijijini na baadaye mapromoter wakamwona sasa hashikiki. Ilikuwa hivyo hivyo kwa akina Diamond na Lulu. Nakushauri anza kuelezea simulizi na tamthilia yako mashuleni – kupitia Fema Clubs, kwenye kumbi za starehe, sherehe za kitaifa na redio za jamii hapo Mtwara labda jitanue mpaka Lindi, Masasi na Tunduma. Kisha onyesha kazi zako za huko kwa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA) ambao wanaweza kukupa fursa kuonyesha kwenye matamasha yao ya kila mwaka. Kwenye matamasha na mikusanyiko ni mahali ambapo unaweza kukutana na watu wa aina na sifa mbalimbali. Unaweza kukutana na wachapishaji au mapromota, huwezi jua. Kizuri kinajiiza, hivyo kama kazi zako ni nzuri kweli utaona zinapata wadhamini au utapata ushauri wa namna ya kuziboresha.

Habari yako Anko Pesa. Naitwa Salmin Yusuf Hamis, nasoma kidato cha 4. Nilikuwa nimefungua genge ambalo ndilo linaloniingizia kipato ili nilipie masomo yangu. Sasa nimeingia kidato cha 4 nitakuwa bize sana, sijui nitaendeleaje, naomba unishauri.

Habari Salmin na pongezi sana kuanzisha mradi unaokusaidia kwenye masomo. Nakushauri usiuache, kwani ukikosa mahitaji muhimu pia itakuwa vigumu kwako kusoma. Kitu unachotakiwa kufanya hapa ni kujua namna ya kutunza muda wako. Angalia ni wapi unapoteza muda wako na utumie vizuri zaidi kuongeza tija kwenye masomo na genge lako. Kuna usemi kwamba angalia sana na kuokoa sekunde unazopoteza kwani ukiokoa sekunde masaa yatajiokoa yenyewe.

Pia angalia uwezekano wa kumfundisha na kumweka msaidizi ambaye anaweza kuendeleza genge wakati masomo yamekubana. Masomo kwanza. Inapofika ule wakati ambao masomo yamepamba moto basi unaweza kufunga genge kwa wiki hiyo na kuendelea nalo baada ya hapo. Kumbuka, kuna maisha baada ya form 4.





Shikamoo Anko Pesa. Mimi naitwa Goodluck na nimehitimu kidato cha nne. Nina miaka 19. Kwa bahati mbaya sikufanikiwa kuendelea na masomo ya kidato cha 5 kwakuwa nilipata division 4 ya 26. Nifanyeje ili nisikae mtaani kama vijana wengine? Nifanye biashara au niapply chuo?

Habari gani Goodluck! Kwanza nianze kwa kukupongeza kwa kumaliza kidato cha nne. Nakupongeza kwa kuangalia fursa mbalimbali za kujiendeleza kimasomo nami sikushauri wewe na vijana wengine "kukaa mtaani" bila kujiendeleza kimasomo. Naambiwa hapa na wenzako ambao umemaliza nao form 4 kwamba division 4 ya point 26 utakuwa na wastani wa C mbili na D tano. Kama huo ni wastani wako unaweza kupokelewa form 5 kwenye baadhi ya shule binafsi aidha kama private candidate au ukarudia somo moja la D ukiwa umeanza A-level ili kulipandisha kuwa C.

Pia unaweza kujiunga kwenye vyuo na kuanza kufanya cheti, kisha diploma, na hatimaye kuchukua degree na wenzako weliokwenda form 5.

Pia, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kinatoa course ya msingi (foundation course) ya kuwezesha wahitimu wa form 4 ambao alama zao hazikutosha kuingia kidato cha 5 kupata sifa ya kusoma degree. Kwa taarifa zaidi kuhusu kozi hii tembelea vituo vya OUT ambavyo viko kila Mkoa (muulize Afisa Elimu Mkoa) au tembelea www.out.ac.tz (au uliza mwalimu mlezi wa Fema Club kwa msaada zaidi).



Shikamoo Anko Pesa. Mimi ni kijana wa miaka 19 na ndoto yangu ni kuwa msanii wa kutengeneza muvi za katuni hadi kufika Disney company. Nifanyeje ili kutimiza ndoto yangu? Nuzzarney, Kigamboni.


Habari yako Nuzzarney, na habari za Kigamboni? Kama ulivyosema hiyo ni ndoto yako na kila mtu ana haki ya kuwa na ndoto yake yenye maono mapana kadri anavyoweza. Sasa basi, katika ndoto hiyo, weka malengo na mikakati ambayo lazima iwe na uhalisia na yenye muda maalum. Anza kwa kusoma masomo ambayo yatakupa mwanga na ujuzi wa kitaalam katika fani hiyo, inaweza kuwa masomo ya sanaa kama lugha na uandishi, au ya sayansi kama kompyuta na upigaji picha.

Unaweza pia hata sasa ukaandika hadithi zako za katuni kisha waone wenye magazeti waombe waanze kuzichapisha. Pita vyuoni, onana na wanafunzi wanaosoma kozi za kompyuta waambie wakitengenezee muvi fupi fupi za katuni. Anza kuzituma Youtube au Instagram kisha zungumza na baadhi ya vituo vya television, waombe wazirushe, kwani vituo vingi hadi sasa tunaona vinarusha katuni za nje tu. Kama zina ubora, tafuta wadhamini wa katuni zako kutoka kwa makampuni yanayozalisha bidhaa zanzotumiwa na watoto kama Azam Ice Cream, Coca Cola, Dar-es-Salaam Zoo, Fun City nk ili zirushwe kwenye TV. Ukimaliza kuufanyia kazi ushauri huu tuje kuzungumza Disney world.

Hongera kwa kazi nzuri Anko Pesa, mimi ni kijana wa miaka 21, niko Njombe najishughulisha na ufundi seremala ila natamani sana kufanya biashara, hasa ya nguo. Lakini, mara nyingi huwa naingiwa na woga hadi kufikia kughairi kabisa, yani nakata tamaa. Naomba unisaidie.

Neno "ujasiriamali" ni mjumuiiko wa maneno mawili – "ujasiri" wa "mali." Neno woga halina nafasi katika ujasiriamali. Ila usiingie tu kwenye biashara mpya bila ya kuisoma ili kuweza kuimudu. Ninachokushauri ni kwamba usiache useremala ghafla na kuanza biashara ya nguo ambayo huijui. Fanya zote kwa kipindi cha mpito ili hii ya useremala unayoijua zaidi ikusaidie wakati ukijaribu kuifahamu na kujenga msingi wa kufanya ile ya nguo ambayo unaipenda sana moyoni mwako. Kumbuka kuweka kumbukumbu za mapato na matumizi kwa biashara zote mbili ili uone ni wakati gani mapato ya biashara mpya ya nguo yanakuwezesha kujikimu. Nasema ondoa hofu kwani mara nyingi watu hufanya vizuri kwenye biashara wanazozipenda.









AKIWA ANACHORA MCHORO WA MASHINDANO



BAADA YA WIKI MBILI...



NDIO... BELITA... MWANANGU AMESHINDA? SHILINGI NGAPI?



MWANANGU AMEULA EE! KUMBE KUCHORA KUNALIPA



HONGERA MWANANGU KUMBE HATA FANI ZA SANAA ZINALIPA



Umakini katika fani

NA RAPHAEL NYONI

Duniani tuko wengi; wa aina tofauti, tabia tofauti na vipaji tofauti. Na ukiacha mahitaji ya msingi, yale mengine nayo yana tofauti. Kwa maana hiyo basi, hata kazi tunazozifanya haziwezi kufanana. Hatuwezi wote kuwa walimu, lazima kuwe na wanafunzi pia.

Wote hatuwezi kutengeneza mabasi au ndege, lazima wawepo wa kuziendesha. Kuna fani ambazo wazazi wengi wangependa watoto wao wazichagua, udaktari, uhandisi, uanasheria, na nyingine kama hizo, sio mbaya hata kidogo, lakini je, ni sahihi kumnyima mtu fursa ya kutumia kipaji chake?

Mara nyingi tunapofikia wakati wa kufanya maamuzi juu ya aina ya taaluma ambayo tunataka kuchagua, wazazi huwa na mchango mkubwa sana katika kufanya maamuzi hayo. Uamuzi wa taaluma ya mtu unaweza ukajenga au kubomoa muelekeo wa maisha ya mtu.

Wapo wengi kama Belita

Belita ni mfano tu wa vijana wengi wa Kitanzania ambao bado wapo shuleni na wanapitia wakati mgumu katika kufanya uamuzi juu ya fani watakazozichagua. Wanajikuta katika mvutano kati ya taaluma wanayoipenda na taaluma ambayo wazazi wangependa wawe.

Ni vema kusikiliza ushauri wa wazazi lakini itakuwa poa zaidi kama utawauliza kwa nini wanakushauri uiendee hiyo fani. Kama na wewe una uchaguzi tofauti na wao, waambie kwa hekima ni kwanini unatofautiana nao na nini kinakufanya uamini katika fani ya chaguo lako.



Muhimu kuwa makini

Unapochagua fani usiangalie tu kama inalipa, usije ukasema na wewe unataka kuwa mwanamuziki au mchoraji kwa sababu tu 'inalipa' au kwa kulinganisha na mafanikio ya mtu mwingine na kudhani na wewe utafanikiwa hivyo hivyo. Angalia kitu unachokipenda na unachokiweza.

Tukirudi kwenye stori ya Belita, kwa kinge' wanasema she is one in a million. Pengine si kila mmoja atafanikiwa kama yeye, lakini pia usipojaribu kuingia katika fani unayoipenda hauwezi kujua ni tuzo gani huko mbele inakusubiri. Kila fani inalipa kivyake.

Unaweza pia ukaanza kwa kujifunza fani moja na baada ya kuwa mahiri katika fani hiyo ukaongezea na fani nyingine pia. Ndiyo, inawezekana, ilimradi tu uwe na subira na nidhamu katika kujifunza bila ya kuharakia mambo.



KUMBUKA

Usione aibu kuhusu taaluma ambayo umeichagua. Wekeza katika kujifunza zaidi ili kufikia ndoto zako kwani kipaji bila shule ni sawa na tairi ya baiskeli bila upepo, utakwenda lakini kwa kuchechemea na wazazi hawatakuelewa.

MAGILA FEMA CLUB NA FILAMU YA KIBABE!

Ni filamu moja kali inayokwenda kwa jina NIMEKOSA NINI!? Kwa hakika, unapoitazama mwili unasisimka, akili inadata na kama huna kifua, machozi yatakutiririka!

Filamu hii ni ya kwanza na ya aina yake kutungwa na kuigizwa na Fema Club. "Kila kitu kuanzia utunzi, uigizaji, shooting, editing mpaka tunatoa CD- tumefanya sisi wenyewe," anasema Mwalimu Yohana Anthony Peter, Mwalimu Mlezi wa Magila Fema Club iliyoko Tanga.

NIMEKOSA NINI!? ni filamu inayoelimisha kuhusu ukatili wa kijinsia, hususan ukeketaji. "Tulipata wazo hili baada ya kusoma Jarida la Fema, toleo lililohusu ukatili wa kijinsia, tukaitazama jamii yetu, tukaona nayo imejaa vitendo vya ukatili dhidi ya mtoto wa kike. Tukasema si vibaya tukatoa kitu ambacho kitaelimisha jamii kwa mtindo wa elimu burudani, yaani edutainment, kama lilivyo jarida la Fema, anasema na kuongeza, "TUKAFANYA KWELI!"

Filamu hii inayomhusu binti Tunu, inaleta nguvu na hamasa kubwa kwa jinsi inavyohitimishwa, kwani linaonekana kundi kubwa la 'Askari wa Fema, wakiwa katika fulana za Fema, wakijitosa kuingia porini kumwokoa binti ambaye almanusura afanyiwe ukatili wa kiwango cha juu".

"Tulifanya hivyo kuonyesha kuwa sisi Fema ni 'wanajeshi'. Sisi si wanajeshi wenye bunduki, la hasha. Silaha yetu sisi ni mdomo. Tunapaswa kuongea, kuelimisha, kukemea na kuripoti vitendo vya ukatili wa kijinsia kila tunaposikia au kushuhudia. Hatupaswi kunyamaza wala kuvifumbia macho. Ndio sababu katika filamu hii utaona 'Fema Soldiers' na ingawa ilikuwa ni katika mazingira magumu, walifanikiwa kumwokoa binti Tunu", anasema Mwalimu Yohana.

Femina inatoa pongezi nyingi kwa Magila Sec kwa kuwa club ya kwanza kutengeneza filamu itakayotumika kuelimisha jamii. Sisi hapa Femina, tulitenga muda, tukakaa kitako na kuitazama filamu hii mwanzo mwisho! We were truly moved! Hongera sana Magila!

Wakati tukiandaa toleo hili kuhusu sanaa na ubunifu, tukasema naam! Magila ni mfano wa kuigwa. Kumbe Fema Clubs zinaweza kutengeneza bidhaa za kuelimisha jamii kulingana na mazingira yao na kwa kufanya hivyo mnaibua vipaji vya wanafunzi katika sanaa ya utunzi, uigizaji na utengenezaji wa filamu kwa ujumla wake. HONGERA!



Unatamani kupata copy yako ya CD? Wasiliana na Magila Fema Club mentor kupitia 0714386338





NAFASI ART SPACE



NAFASI Art Space, in Dar es Salaam, was set up to create a platform where artists can meet, exchange ideas, learn and search for opportunities together. So far there are 32 studios and more than 60 artists active in the space. One of them is Muda Africa which trains youth on song and dance and organizes study tours and exchange programs that take local artists abroad to give them exposure, and invites artists from abroad to Tanzania for dynamic exchange and collaboration. The NAFASI art space earns its income from art exhibitions of visual art and performances of dance and song, but also receives support from different donors.



Different government and non-governmental organizations are working together with NAFASI to train and expose local artists to international standards. "We have strong collaboration with BASATA, COSOTA and Tanzania Film Board", Agness Senga explains, she is the Business and Marketing Officer at NAFASI. "We are not getting any financial support from the government, but its regulatory authorities have been very supportive to strengthen ethics in all arts under our wings".

Nafasi Art Space was established in 2008, by a group of five passionate culture lovers namely; Sauda Simba, professor Elias Jengo, Davies Kitururu, Sandra Mushi and Demere Kitunga. Congratulations to this group of enthusiasts who have contributed to the development of the arts in Tanzania!



Till this day, NAFASI Art Space continues to empower youth, even children, to use their artistic talents to express their ideas and feelings. Many are also learning how to generate income from their art.

SWAHILI FASHION

In Tanzania, the word Fashion is strongly associated with SWAHILI FASHION WEEK, set up in 2008. At this event, which runs for three days every December, 'fashionistas' - fashion lovers, gather from near and far. Aspiring designers can showcase their creativity, get exposure, network with people in the industry from all over east Africa and elsewhere. They can also receive Awards for their work! It has stimulated a revolution in clothing design, clothing accessories like hats, bags, jewellery and shoes as well as for fashion modelling in the region.

The legendary fashion mentor Mustapha Hassanali, is behind the event. He is a medical doctor by training but left his profession due to his love for fashion! What a blessing that was, he has instead transformed the business of fashion in Tanzania and created huge opportunities



/ SWAHILI FASHION WEEK

for young Tanzanians to excel in the business. SWAHILI FASHION WEEK is according to Hassanali, stimulating many employment opportunities for young people.

Every year the fashion week offers 10 young designers the chance to be mentored, helping them to grow from one stage to another, as they participate in challenges before and during the fashion week.

Volunteering with the SWAHILI FASHION WEEK is also possible. There are opportunities for 30 youths to apply to assist in different sectors including stage setting, different services in the media and marketing departments as well as in fashion coordination. Volunteering always 'pays' as it provides chances to get exposure and networks, invaluable in any field.

So! If you are interested in fashion, this is the place to be!



SEMA. TENDA!



Sanaa na misingi yake

NA AMABILIS BATAMULA

Sema.
Tenda!



Dulvanni akionyesha
sura zake tofauti za
kuchekesha



Unajua, kila shule ina angalau mwanafunzi mmoja ambaye kila mtu anamfahamu. Wengine wanafahamika kwa kuwa vinara wa fujo na wengine kwa kuwa washiriki wa kila jambo linalotokea shuleni. Wapo wale wengine sasa, ambao kila akikaa kundi hiloo limemzunguka! Eeeh, hivyo ndivyo ilivyokuwa kwa Abdallah Sultan, alipokuwa shule, hasa pale Tabata High School. Stori juu ya stori. Wengi sasa tunamfahamu kama Dulvanni, msanii wa vichekesho.

Anafahamika zaidi kwenye mitandao ya kijamii, lakini siku si nyingi zijazo, Dulvanni (21) ataonekana zaidi kwenye runinga. Hivi karibuni aliingia mkataba na DStv, ataonekana Afrika nzima. Ndoto yake ya kuwa maarufu ndo kwaaaaanza inashika kasi. Dulvanni amewahi kufanya kazi na washanii kama Diamond Platnumz, amefanya matangazo ya kampuni za simu na ameshiriki katika Fema TV Show.



Mambo yalianzaje?

HAHA!
HAHA!

“Matokeo yangu ya kidato cha nne hayakuwa mazuri, hayakuniwezesha kuingia kidato cha tano. Lakini nilitambua kwamba elimu ni muhimu sana kwangu, hivyo niliamua kusomea uandishi wa habari ngazi ya cheti. Mtazamo wangu ni kwamba kuchanganya uchekekeshaji na uandishi wa habari kutanisaidia”.

Dulvanni amekuwa akifanya sanaa ya vichekesho kwa muda mrefu lakini hivi karibuni ndio ameamua kuwa serious na jambo hilo. Mwanzoni alikuwa akiigiza nyimbo kali za wasanii mbalimbali, zikitoka tu anazifanyia video zenye vituko vya kuvunja mbavu, halafu anapandisha mtandaoni, watu wanaenjoy. Lakini lengo lilikuwa kwenye kutengeneza brand yake mwenyewe yenye vitu vipya, alivyotengeneza kutoka mwanzo. Dulvanni anafahamika kwa kucheza nafasi ya wahusika wawili, mwanamke na mwanume. “Watu walikuwa na maswali mengi mwanzoni “ilichukua muda nikawaelewesha kwamba ni sanaa tu.” Haikutokea tu nikaanza kuigiza nafasi ya watu wawili, kulikuwa na sababu. “Kuna wakati nilikuwa naigiza na watu wengine, bajeti zenyewe ndogo, nikiwasubiri hawatokei, nikaamua kuwa mbunifu na kucheza nafasi mbili. Nitaifanya chochote kusababisha watu wacheke.”



Dulvanni na Femina Power Teams wakiigiza katika Fema Tv show

TIRIRIKA

Unafahamu nini kuhusu BASATA?



MARIAM MAGANGA (16)
Shinyanga

Ni shirika ambalo linasimamia kazi za wasanii na kuhakikisha wanatunza maadili ya Mtanzania katika kazi zao za sanaa na hata maisha yao ya kisanii popote pale wanapokuwa.




BILICRINTON RUBUNDA (19)
Kagera

Ni Baraza la Sanaa Tanzania ambalo husimamia na kutunza heshima ya sanaa kwa ujumla na kutoa adhabu kwa wale ambao wameingia kwa ajili ya kuidhalilisha sanaa.



OMARI FADHILI HAMISI (17)
Tanga

Inasimamia wasanii, kuhakiki na kupitisha kazi za sanaa. Baraza hili pia lina mamlaka ya kufungia kazi yoyote ya sanaa itakayoonekana kuwa haizingatii maadili.





Ubunifu wake na utayari wa kujaribu vitu vipya ndiyo mambo yaliyomsaidia kujenga jina haraka. Dulvanni ni shabiki mkubwa wa wachekeshaji maarufu kama Joti, Kevin Hart, Mr Bean na Charlie Chaplin. "Mastaa hawa wamenionesha kwamba kwenye komedi lolote linawezekana. Na tangu nikiwa mdogo nilitamani kuwa kama wao." Anasema.

"Sasa nimepata mwanga," anaongeza, "lakini pia nimegundua kwamba ili uwe maarufu unapaswa kufahamu na

kuwajibika kwa kile unachokifanya." Dulvanni anaamini kwamba ili kazi yake iwe nzuri inapaswa iendane na mazingira na mahitaji ya hadhira. Ni muhimu kuzingatia maadili katika kazi za sanaa. Bila hivyo unakuwa haujengi bali unabomoa, pia kazi yako inaweza isikubalike. "Ninajifunza kwa waliokosea na kwa ambao hawakukosea, yote ni mafundisho mazuri, napenda nifike mbali sana."

Dulvanni akiwa na Mc Pilipili katika moja ya matamasha ya ucheekeshaji



Akapata mwongozo

Katika pilikapilika zake za ubunifu na za uvumbuzi, na katika kutafuta namna ya kujiingizia kipato kutokana na sanaa ya ucheekeshaji, Dulvanni amejisajili BASATA yaani Baraza la Sanaa la Taifa. Hii ni taasisi ya serikali ambayo ina mamlaka ya kisheria ya kusajili wasanii nchini. "Nilitaka kuelewa mchakato ambao ungeniwezesha kuendesha shughuli zangu kihalali na kufanya sanaa bila wasiwasi," anaeleza.

Walinishauri namna gani naweza kukua katika sanaa na kuhakikisha kwamba maudhui yangu na lugha ninayoitumia

inakubalika. Napaswa kuwasilisha kazi zangu BASATA ili nipate mrejesho wao na nimekuwa nikipewa ushauri kuhusu mambo kadhaa, kwa mfano namna ya kusajili kazi zangu COSOTA ili niwe na hakimiliki. COSOTA ni taasisi ya serikali inayosimamia hakimiliki za wasanii. Pia nimegundua kwamba BASATA inaweza kukutetea ikiwa haki zako kama msanii zinaporwa.

Baadhi ya watu wanasema kwamba BASATA ni kikwazo kwani inawachelewesha wasanii, hivyo inawachelewesha mafanikio na kwamba inawapunguzia uhuru. Dulvanni anasema yeye hajakutana na kikwazo chochote katika kufanya kazi na BASATA. Anasema "sisi kama wasanii tunapaswa tuzoe utamaduni wa kupewa ushauri, kukosolewa na kuheshimu hisia za hadhira yetu. Tuache siasa".

Mawazo yake yanashabihiana na maelezo ya Katibu Mtendaji wa BASATA, Godfrey Mngereza, "moja ya kazi za Baraza ni kukosoa kwa lengo la kuboresha, hatukosoi kwa lengo la kumkwamisha mtu au kuchelewesha mafanikio yake. Unajua popote duniani kwenye tasnia ya sanaa kuna watu wanaitwa critics, unawapa kitabu chako au mashairi yako au kazi yoyote wanaipitia wanakupatia mrejesho".

"Ili ufike unakotaka, unapaswa kuelewa na kuzingatia misingi ya sanaa," anaeleza Dulvanni. "Naamini katika kusonga mbele. Sitaki chochote kinirudishe nyuma. Nataka kufika mbali katika sanaa hii ya vichekesho."

Kuhusu BASATA

- ★ Ni Taasisi ya Serikali inayosimamia maendeleo ya sanaa zote nchini. Inawashauri wasanii katika nyanja zote za sanaa. Inasajili wasanii na kuwapa leseni za kufanya kazi za sanaa.
- ★ Ili kikundi au msanii asajiliwe anahitaji kuwasilisha wasifu wake au wa kikundi, picha pamoja na kujaza fomu ambazo zinapatikana ofisi za utamaduni wilayani, BASATA makao makuu na kwenye tovuti www.basata.go.tz.
- ★ Gharama za usajili ni 45,000/= kwa msanii binafsi, 85,000/= kwa vikundi na 115,000/= kwa studio za kuzalishia muziki. Unaweza pia kusajili ukumbi wa starehe.
- ★ Ni kosa kisheria kufanya kazi za sanaa bila kusajiliwa BASATA. Kufanya hivyo ni sawasawa na dereva anayeendesha gari bila leseni.
- ★ Linawajengea uwezo wasanii kupitia warsha, matamasha, ziara za kirafiki ndani na nje ya nchi na sasa limeanzisha mpango wa kuwalipia ada wasanii wa kike katika Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa) ili kuongeza idadi ya wasanii wanawake wenye mafunzo. Mwaka huu wapo sita.
- ★ Kwa kushirikiana na Baraza la Mitihani la Taifa, BASATA inatoa tuzo ya fedha kwa wanafunzi wanaofanya vizuri zaidi katika masomo ya sanaa zote ikiwemo muziki, uchoraji, uchongaji na sanaa za maonesho, kwenye mtihani wa kumaliza kidato cha nne.

The Rules of Art

BY AMABILIS BATAMULA

HA! HA!
HA!

Every school has that one student everybody knows, the really popular one. Some get that reputation because they are trouble makers, others because they get involved in everything that happens at school. And then there are crowd pullers, like Abdallah Sultan was at Tabata High Secondary School. He always had a story to share and a crowd around him ready to listen! He is now known as Dulvanni, the comedian.

Already popular on social networks, Dulvanni (21) will soon be seen on television. Recently he signed with Dstv and will appear on TV screens throughout Africa. His dream of becoming famous is just gaining momentum. He has already worked with artists like Diamond Platnumz, done ads for phone companies and has been part of the Fema TV Show.

So how did it all begin?

"My form four results were not impressive and couldn't get me into high school, but education is important to me, so I took a certificate course in journalism instead. My thinking is that combining comedy and journalism will help me".

Dulvanni has been doing comedy for a long time, but it's just recently that he decided to try it as a career. When he started, he would act out funny videos for new hit songs by various artists and would upload them online. But he wanted to create his own fresh material.

He is known for playing double characters, female and male, in his comic skits. "People had a lot of questions about that in the beginning, it took time to make them understand it was just 'art'. There was a reason for why I started to play double roles. At the time I was producing on small budgets, I had to bring in other people to act with me, but sometimes they wouldn't show up, I had to get creative and play two roles. I'll do anything to provoke and make people laugh".

Amazing creativity and his willingness to try new things has helped him build a name quickly. He is a great fan of comedians like Joti, Kevin Hart, Mr Bean and Charlie Chaplin. "These comedy stars showed me that everything is possible in comedy and since I was a kid I wanted to be like them, says Dulvanni.

"Now I've seen the light," he adds, "but I have also realized that to become popular you have to be aware and take responsibility for what you say." Dulvanni believes that for one's work to be good, it has to reflect your audience's realities and preferences. It

is important to embrace good values and ethics in artistic works, because ignoring that can be counterproductive; your work can be rejected or banned. "I'm learning from those who got it wrong and those who got it right. They all teach me something on my journey".

Getting guidance

In his creative exploration, trying to understand how he could make an income of his comedy, he has registered with BASATA, the National Arts Council. This is the government institution that is legally tasked with registering artists in the country. I wanted to understand the processes that will allow me to legally and smoothly navigate the world of art" he explains. They gave me advice on how to grow artistically and make sure that my content and language use is acceptable. I have to submit my major projects to BASATA for feedback and I have been advised on a few things, like how to register my work with the copyright society, COSOTA – a government institution that protects artist's intellectual property rights. I also learned that BASATA can defend you if your rights as an artist are being violated. "

Some people say that BASATA is an obstacle delaying artists' ability to operate and therefore their success, that it can limit 'artistic freedom'. So far Dulvanni has not experienced that in any way, he comments "as artists we should embrace the culture of receiving critique and be aware of our audience and respect their feelings. Avoiding politics is also good advice".

His thoughts echo those of BASATA Executive Secretary, Godfrey Mngereza, "one of the functions of the Council is to provide advise by critiquing art for the purpose of improving it, not to discourage the artists or delay their accomplishment. Globally in the art industry there are people called critics, you give them your lyrics, your book or any work of art, they review it and give you feedback"

"You have to understand the rules of the game to get there", explains Dulvanni. "I believe in progress, in moving ahead, I don't want anything to hold me down. I want to go far in this comedy career."

About BASATA

- ★ It is a Government institution that oversees development of the arts in the country. It advises stakeholders on all aspects of art and registers artists issuing them licenses to operate.
- ★ For a group or individual artist to register, they need to submit their profile, photographs and fill out forms that are available at cultural offices in the district, BASATA headquarters and at www.basata.go.tz
- ★ Registration fees are 45,000/= for individual artist, 85,000/= for groups and 115,000/= for music production studios. You can also register recreation halls.
- ★ It is an offense to operate without BASATA registration, doing so is similar to driving without a license
- ★ Provides capacity building to artists through workshops, festivals, cultural exchange programs locally and internationally. It gives out 6 scholarships to promote female artists at the Bagamoyo Institute of Arts (TaSUBa).
- ★ In conjunction with the National Examinations Council, BASATA awards best students at form four level in all art subjects including music, painting, sculptures and performing arts.



Power Teams katika Ubunifu

NA GEOFFREY MACHEMBA

Mpo 'fire' au mmepoa? Sisi hapa mjengoni hatupoi kabisa. Kwanza, kwa niaba ya team za Nguvu ya Binti na Nguvu ya Kaka niwakaribishe katika kurasa maalum za Power Teams. Tunazidi kukua eeh? Basi tutakuwa tunakutana hapa katika kila toleo kuanzia sasa tukiongelea mawili matatu kuhusu Power Teams.

Kama mliyooona, toleo hili linaimulika tasnia ya ubunifu. Katika tasnia hiyo na sisi power teams hatuko nyuma. Si mnakumbuka tuliwaambia timu hizi zinajumuisha vijana kumi wa 'backgrounds' tofauti? Basi tupo kadhaa katika sekta ya ubunifu, lakini leo acha niwakilishe!

Naitwa Geoffrey Mchemba. Nina vipaji kibao katika sekta hii ya ubunifu: Mimi ni mbunifu wa mavazi, mwigizaji, mwimbaji na pia ni mtangazaji, subiri muone mambo yangu katika msimu wa 12 wa Fema TV show.

Nilipoanzia

Niligundua na kuanza kufanyia kazi vipaji vyangu nikiwa shule. Nilikuwa nikishiriki katika matamasha mbalimbali yakiwemo ya Fema club kwa kufanya ubunifu wa mavazi kwa ajili ya fashion show na nilifahamika sana kwa hilo. Baada ya kuhitimu mwaka 2016 nikajikita rasmi katika kutumia vipaji vyangu. Nikajiunga na kikundi cha maigizo kilichoitwa Millrose, kupitia kikundi hicho nikashiriki katika filamu inayoitwa "Chozi la Yatima".





Baada ya hapo nilijiunga na Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) nikichukua Diploma ya Bima na Udhhibiti Majanga. Umeona nilivyokwenda nje kabisa ya vipaji vyangu? Lakini hiyo haikunifanya nisiendeleo kuvifanyia kazi na kupigania ndoto zangu. Mwaka 2018, nikahitimu chuo, na mbio zikaendelea. Nilianza na mtaji mdogo sana wa vitenge viwili tu, nilibuni mitindo, nikashonesha na kuuza. Taratibu nilijiongeza mpaka kufikia sasa nina jumla ya cherehani 5, nimekodi frem na kuingia makubaliano na mafundi. Brand yangu naiita "Geoafrica", ambapo tunabuni, kushona na kuuza nguo zitokanazo na vitambaa vya kiafrika kama vile vitenge na khanga.

Mchumia Juuni...

Haikuwa rahisi kufikia hatua hiyo. Nilipitia changamoto nyingi sana, baadhi bado zipo mpaka sasa. Mojawapo ni ukosefu wa mtaji wa kupanua biashara na ukosefu wa masoko, lakini pia siwezi kusahau changamoto kama vile kukatishwa tamaa na baadhi ya watu kwa sababu hata wazazi na ndugu hawakuwa wanaamini kuwa ninaweza kutengeneza maisha kupitia vipaji vyangu. Wengine walidhani nitapoteza dira na nitakuwa mhuni, hivyo zoezi gumu la kwanza lilikuwa ni kuwashawishi wakubaliane na maono yangu. Nilipambana bila kukata tamaa. Kuna wakati nilitembea kwa mguu umbali mrefu, nilishinda na njaa nk, yote hayakuwa vikwazo vikubwa kwa sababu nilikuwa natazama mbele.

Nilipata nafasi ya kujitolea hapa mjengoni Femina Hip na kutokana na kuona shughuli zangu, nikateuliwa kuwa mmoja wa timu ya Nguvu ya Kaka, na nikaenda mbali zaidi kwa kuteuliwa kuwa mtangazaji wa vipindi vya Fema TV show, sanjari na Lydia Charles, kiongozi wa timu ya Nguvu Ya Binti. Hapa sasa napata fursa ya kukitumia vyema kipaji changu cha utangazaji, kwa mantiki hii, Femina inanisaidia

kukuza vipaji vyangu, nikudokeze tu, hata nguo ninazovaa kwenye Fema TV show, nimebuni mwenyewe na kushona kwa kutumia khanga za miaka 20 ya Femina Hip. Naamini kila mtu ana kipaji. Kikubwa tengeneza ndoto yako na uifanye kazi. Kama una kipaji katika sekta kama za kwangu basi karibu sana. Ushauri wangu ni kwamba kama ukumbana na vikwazo, usikate tamaa, pambana. Kama wazazi hawaelewi unachofanya, zungumza nao kuhusu maono yako, ikibidi fanya kwa bidii ili waone faida ya kile unachokifanya. Binafsi bado nina safari ndefu lakini nina imani NITAFIKA.

**Wakati unasubiri kusoma
kurasa za Power Teams toleo lijalo,
hebu fuatilia na ushiriki
mjadala yetu katika social media:**

Instagram @feminahip

Twitter @feminahip

Facebook @feminahip

**KILA JUMATANO
YA MWISHO WA MWEZI**

KWA TAARIFA SAHIHI, ELIMU NA USHAURI KUHUSU AFYA, VVU NA UKIMWI

Piga **117**

24H
L I V E
SUPPORT

SMS



Piga simu bila malipo
kwenda namba **117**

Au tuma neno AfyaEdu kwenda
namba **15017**




info@tayoa.org • www.tayoa.org/www.vijanatz.com





CHALENJI NO. 25



Naam! Zile Club Challenge zetu za kawaida zimerejea. Na safari hii tuna habari njema kwenu. Idadi ya washindi kwa kila toleo imeongezeka, **kutoka mshindi mmoja hadi sita** na lengo ni kuongeza wigo wa ushindi kwani washiriki ni wengi.

Wanashinda nini?

Ongezeko hili la idadi ya washindi ni kuanzia Club Challenge no 24! Mshindi wa kwanza (mmoja) atashinda zawadi kubwa kabisa ambayo ni kuhudhuria Youth Conference Jijini Dar es Salaam, tisheti 20 za Femina na pair moja ya khanga. Washindi wengine watano watahinda pair moja ya khanga matata kabisa ya miaka 20 ya Femina (pair moja kwa kila club). Yes! Tunafahamu kwamba mnahitaji khanga kwa mapambo na branding mnapokuwa katika shughuli zenu za club. Au vipi?

Tujikumbushe chalenji no 24

Chalenji hii ilitangazwa katika toleo no 49 lenye cover ya Jokate Mwegelo na iliwataka mfanye mjadala uliohiba kuainisha changamoto zinazowafanya wasichana washindwe kumaliza shule, kisha mtuandikie ripoti tamu ya mjadala na muambatishe na picha za mjadala.

Mlitisha kinyama!

Aisee! Kuna waliofanya mjadala kwa kuhusisha shule nzima, kuna waliokwenda mbali zaidi na kutafuta takwimu za wasichana walioacha masomo mwaka juzi na mwaka jana na sababu za kuacha masomo, wapo waliojiongeza zaidi wakafanya mahojiano na wazazi na uongozi wa serikali ya kata, wengine wametisha kabisa wakarekodi videoz zinazoonyesha namna walivyofanya chalenji hii! Aisee. Hata kuamua washindi halikuwa zoezi rahisi. Nyinyi nyote ni wakali!

Washindi Wetu Kwa Chalenji No 24 Ni

SENGA SEC SCHOOL.

Huyu ni mshindi wetu wa kwanza. Senga Fema Club wanapatikana Geita. Wao walifanya mjadala wa kibabe uliohusisha shule nzima. Walialika walimu pia ili hoja zinazojadiliwa hapo zifanyiwe kazi kama ziko ndani ya uwezo wa shule. Katika ripoti yao wameainisha sababu kumi zinazopelekea wasichana kushindwa kumaliza masomo yao na pia wameorodhesha mapendekezo kumi ya nini kifanyike ili kutatua changamoto hizo. Kama hiyo haitoshi, wametuma pia still pictures na videos za kibabe! Big up sana SENGA SEC SCHOOL. Anzeni tu kupanga watakaowawakilisha Dar katika Youth Conference 2020!



ZAWADI KWA SENGA SEC

- * Kuhudhuria Femina Hip Youth Conference 2020
- * Tisheti ishirini za Femina
- * Femina khanga (pair moja)

WASHINDI WENGINE WATANO NI

- * Mnero Sec School – Lindi
- * Nkome Sec School – Geita
- * Matai Sec School – Rukwa
- * Kwiramba Sec School – Mara
- * Businda Sec School - Geita

Pongezi nyingi kwenu, tutawasiliana nanyi tuwatumie khanga matata ya miaka 20 ya Femina.

HII HAPA CHALENJI NO 25

Tunafahamu kwamba shule kibao zina Fema Club Smart Areas! Yaani kaeneo fulani hivi ambako mmepeva na uongozi wa shule, mmekaremba mtakavyo, labda kwa chupa za plastiki, kwa mawe, wengine maua, nk na mnakatumia kwa mikusanyiko yenu ya hapa na pale. Enhee, hapo hapo! Wengine mnaita Fema Club Smart Space, au Fema Club Corner! Naam.

Sasa: Kwakuwa toleo hili linahusu sanaa na ubunifu na kwakuwa moja ya maeneo yenye ubunifu ni katika upigaji picha, kama mlivyosoma katika kurasa za Ruka Juu. Basi nanyi kama mlivyoweka ubunifu katika kuipendzesha Fema Club Smart Area yenu, wekeni ubunifu wenu pia katika kupiga picha matata za smart area yenu.

Pigeni picha NNE kali zinazoonyesha Fema Club Smart Area yenu na mzitume kwetu. (picha mnato/still pictures. Sio video)

VIGEZO VYA USHINDI:

- * Mvuto wa smart area yenu
- * Ubunifu katika kutengeneza smart area yenu
- * Ubora wa picha hizo nne mtakazotuma kwetu
- * Kuwe na ushahidi wa kuridhisha angalau katika picha moja kwamba hilo ni eneo la Fema Club na si la club nyingine.

KUMBUKA

Kama mtaamua kutuma picha kwa email, zitumwe kama attachment ili zisipungue ubora. Zisitumwe kwa whatsapp wala facebook.

WASHINDI WATAKUWA SITA:

Mshindi wa kwanza (atashinda T-shirt 20, Femina Khanga pair moja na kuhudhuria youth Conference 2020. Washindi wengine watano watajishindia Femina Khanga pair moja kila club.

Ripoti za
CHALENJI no25
zitumwe kabla ya
AGOSTI 15, 2019.
GOOD LUCK!




COMPETE & WIN



JINSI YA KUSHIRIKI:

Hili ni shindano na yeyote anaweza kushiriki. Andika maswali na majibu yako katika karatasi nyingine, siyo kwenye ukurasa huu. Unaweza kutuma majibu yako kwa barua pepe au kwa njia ya posta. Hakikisha umeweka anwani yako ya barua na ikiwezekana weka namba yako ya simu kwa mawasiliano. Majibu ya maswali yote yanapatikana humuhumu ndani ya jarida. Washindi watajinyakulia fulana bomba ya Femina. Changamka!



KULIA

3. Ni mmoja wa vijana wanaounda kundi la The Mafik
4. Ni taasisi yenye mamlaka ya kusajili wasanii nchini
5. Wilaya inayopatikana Kaskazini Magharibi mwa Tanzania
6. Ni mwalimu wa Misungwi Sec
8. Best Fema Club
11. Ni kitu muhimu sana katika mwonekano wa mtu
12. Mlezi wa Mnero Fema Club iliyoko Lindi
14. Safari yake katika taaluma aliyonayo ilianza chuoni
15. Alitambua kwamba elimu ni muhimu sana kwake
16. Best Fema Club Metor

CHINI

1. Ana miaka 34, alizaliwa Dar es Salaam, ni Muha
2. Ndiyo inayotufanya tupendwe na kupata umaarufu
5. Anapenda kudansi, kuimba na michezo
7. Anafundisha Historia na Kiswahili A Level
8. Ni kazi nzuri sana, inalipa, kama ukijenga jina
9. hauji ghafla
10. Mwenyekiti wa Serengeti Network of Fema Clubs
11. Kila mwenye kipaji na anatamani kukiendeleza anamhitaji mtu huyu
13. Mwanzilishi wa Tanga Network of Fema Clubs

MAJIBU YATUMWE KABLA YA AGOSTI 15.
Jinsi ya kutuma: angalia anwani ukurasa wa mwisho wa toleo hili. Washindi wataangazwa toleo no 53.



VUNJAMBAVU

POMBE SI TOGWA!

Mlezi kanunua gazeti, alipofika nyumbani tu akaliweka kwenye friji. Mke wake alipomuona akashangaa, akamuuliza "mbona umeweka gazeti ndani ya friji?" Mlezi akajibu "wameandika lina habari motomoto acha zipoe kiasi ndo nisome." Mkwewe hadi sasa anauguza mbavu zake, maana sio kwa kucheka kule!



MAJINA YA WASHINDI WA TOLEO LA 49

Meshack M. Emmanuel, Azania Sec School, P.o.box 9074, Dar Es Salaam.

Irene Alex Mtui, Mikanjuni Sec School, P.o.box 29, Tanga.

Amos D Emmanuel, Mabonde Sec School, P.o.box 174, Bukene, Nzega.

Godfrey Z. Anthony, Sengerema Sec School, P.o.box 42, Sengerema, Mwanza.

Hadija Athumani, Tongi Sec School, P.o.box 119, Ndala, Tabora.

Naomi Baraka Joel, Bunda Sec School, P.o.box 400, Mara.

Kelvin Malamsha, Chidya Boys High School, P.o.box 324, Masasi, Mtwara.

Bituro M. Kipande, Iringo Sec School, P.o.box 652, Musoma, Mara.

Scolastica L. Edward, Sigino Sec School, P.o.box 680, Babati.

Halima A. Kibetu, Mjawa Sec School, P.o.box 50, Kibiti.



WASILIANA NA FEMINA



Kuna ubunifu katika mawasiliano pia



Ndio maana tunakupa 'options' kibao za kuwasiliana nasi



WEBSITE
www.feminahip.or.tz



FACEBOOK
Femina Hip



TWITTER
@feminahip



INSTAGRAM
@feminahip



YOUTUBE
@feminahip



ANUANI YA POSTA
Femina Hip
S.L.P 2065, Dar es Salaam,
Tanzania



EMAIL
info@feminahip.or.tz



TELEPHONE +255 222 700 742
SMS 0753003001

Una maswali, mrejesho au mapendekezo kuhusu kazi zetu?
Au kuna tatizo lolote la ufikaji wa Fema katika shule yako?
Tuma SMS kwenda **0753003001** kuwasiliana nasi!

16 PEACE, JUSTICE AND STRONG INSTITUTIONS



Ticha MC



femina
hip

SI MCHezo!